

YEYE HUJALI. JE!

WEWE UNAJALI?



Asante, Ndugu. Na tuendeleo kusimama kwa muda kidogo sasa kwa ajili ya maombi. Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu, je! kuna ombi lolote la kutamkwa, ama kutambulishwa kwa kuinua tu mkono wako, kama tu ukiuinua mkono wako hivi, sawa, shikilia tu ombi lako sasa.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakujia tena, kwa ajili ya maombi ambayo... wameiinulia mikono yao hewani. Nao ni wahitaji asubuhi ya leo, Bwana, wa mambo mengi. Wewe unajua wanayowazia moyoni mwao, kwa maana Wewe ni Neno, nalo Neno ni Tambuzi la mawazo na makusudi ya moyo. Nami ninakuomba, Mungu uliye Mwingi wa Neema, ya kwamba utamjibu kila mmoja wao kulingana na mahitaji yao, tukijua jambo hili, ya kwamba Wewe utawajibu kulingana na imani yao. Tupe imani tunaponena Neno Lako basi, Bwana, jalia liwalettee imani. Nisaidie kulinena Neno Lako, kwa kuwa Neno Lako ni Kweli, lipate kuleta imani kutoa jibu kwa maombi haya. Halafu huenda kukawa na wengine hapa, Bwana, ambao wameiacha ile njia nyembamba, wasiotembea katika njia ya Kweli. Tunaomba, Baba, ya kwamba jambo fulani litafanywa leo, na kutambulishwa, wapate kurudi upesi kwenye ile njia ya ushirika na Kristo tena. Siku zinaenda sana, uovu uko kila mahali, kuna kuanguka kuuu. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utajitambulisha kwetu leo, kwa kuwaponya wagonjwa miongoni mwetu, kutenda miujiza. Si kwamba inakubidi kuifanya, Bwana, kutufanya tujue ya kwamba Wewe ni Mungu, bali ni kwa sababu uliahidi kuifanya. Nasi tunajua ya kwamba Wewe utatujalia ahadi Zako kama tu tutaziamini na kujua ni za kweli. Tunaomba majaliwa haya katika Jina la Yesu Kristo. Amina. (Mwaweza kuketi.)

³ Nilikuwa tu nikichukua muda kidogo kusoma baadhi ya maombi yaliyowekwa hapa, kuna mawili ama matatu, moja ni ombi la maombi. Bila shaka, kuna lesa nyingi zimewekwa hapa ambazo tungefurahia ku—kuziombea katika muda mfupi tu, tunapohisi kuwa Uwepo wa Roho Mtakatifu u—umefikia kilele Chake. Hapo ndipo ninapojaribu kuombea hizi, wakati kusanyiko lote, wote wametiwa mafuta kwa Uwepo Wake.

⁴ Tunasikitika sana ku—kuwasumbua, tuna wengi sana wanaosimama, wala hakuna nafasi kwao ya kuketi. Na—na hii ndiyo siku ambayo joto la hali ya hewa imefikia kilele chake cha joto, tuna karibu asilimia mia moja ya unyevu na karibu nyuzi joto mia moja, kwa hiyo kuna unyevu sana na ni joto.

⁵ Nami nilitoa asubuhi ya leo kwa ajili ya ibada za uponyaji, ama sio... Sababu ya mimi kufanya hiyo ibada ya “uponyaji,” ni kwa kuwa ninaiweka imani yangu katika yale Yeye aliyoahidi. Unaona? Sasa, siwezi kusema ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo, bali ninaamini baada ya kulisikia Neno Lake na kuwekea msingi imani yetu juu ya yale ambayo ameahidi, basi tuna haki ya kudai ahadi Zake za uponyaji, kama tu tunavyodai ahadi Zake za wokovu.

⁶ Maombi haya machache. Sijui kama bado wamevifungulia vinasasauti kwa ajili ya huu, ama bado. Huenda likawa ni jambo jema. Vema, nadhani ni vizuri kwa walio nje, jamii kulisikia hili, ni ombi.

Je! ulitabiri ya kwamba kutakuwako na wanegro milioni mo—moja watakaouawa kwenye...ama ulitangaza tu kwamba jambo hili litatokea?

⁷ Sasa, mnaona, daima nimewaomba mwe waangalifu kwa yale mnayosikiliza. Mnaona? Kuna mengi sana ambayo ni upande tu wa kibinadamu. Bali sikuzote kama kuna kitu kinachotukia, kitanenwa, “Ni BWANA ASEMA HIVI,” hata kwa maono ama chochote kile. Maono kwenye jukwaa, katika wasikilizaji, unafanya hivyo mwenyewe; sio Mungu, ni wewe. Unaona? Mungu hatoi ono hilo, unalitoa mwenyewe, kwa imani yako katika karama ya Kiungu.

⁸ Kama yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, Yeye hakujua kwamba alikuwa ni nani ama shida yake, bali mwanamke alifanya hivyo mwenyewe. Unaona? Sasa, hiyo haikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI wakati Yesu alipojibu na kumwambia ya kwamba imani yake ilikuwa imemwoko. Lakini, unaona, inakubidi kuwa mwangalifu.

⁹ La, nilikuwa tu nikizungumza juu ya Martin Luther King, katika maafa haya makuu waliyo nayo huko Kusini, kuhusiana na watu we—weusi. Nilisema, “Kama watu hao wangelikuwa ni watumwa, ningelichukua kanisa langu na kwenda kusini kuwasaidia watu hao watoke utumwani.” Hakika ningeenda, kwa maana mwanadamu hufanya watumwa, sio Mungu. Sisi sote ni wa damu moja. Sote tunatokana na mti mmoja, na hiyo ilikuwa ni kutoka kwa Adamu. Mungu, kwa damu moja, ameyafanya mataifa yote. Na kama sisi, rangi zetu ni hudhurungi, ama nyeusi, ama manjano, ama nyekundu, ama yoyote ile, sisi sote ni viumbe vya Mwenyezi, mnaona, wala hakupaswi kuwepo na tofauti zozote baina yetu.

¹⁰ Swali kule chini ni “ubaguzi wa shule.” Sasa, nilikuwa huko wakati wa maasi ya kwanza, nami niliyasikia, nami na—najua yale ninayozungumzia. Watu weusi wana shule nzuri, wakati mwingine ni bora zaidi kuliko shule hizo zingine. Na, kwa mfano, huko Shreveport wana shule nzuri kuliko za wazungu zilivyo. Lakini ni nia ya mtu fulani kuwachochea ya kwamba

wanapaswa kwenda na kujichanganya nao. Ambalo, nafikiri lingekuwa ni sawa, bali mradi watu wanapinga hilo, hao watu wa kusini, basi inaleta tofauti gani hata hivyo?

¹¹ Nami nafikiri ya kwamba Martin Luther King amevuviwa na Ukomunisti, ambao utawaongoza karibu watu milioni moja kabisa kwenye mtego wa mauti. Unaona? Sisemi ya kwamba Bwana aliniambia jambo hilo. “Mimi” naamini, unaona. Na naamini halipaswi kufanywa. Nafikiri ya kwamba watu wanapaswa kuwa Wakristo na kutambuana kama ndugu. Pia, lakini nafikiri kwa sababu tu...

¹² Hii Marekani, serikali hii sasa inaniambia ya kwamba hata siwezi kutia sahihi cheki ambayo—ambayo itakuwa... nimepewa mimi binafsi. Unaona? Hizo ni haki za kikatiba ambazo nimenyang’anywa, lakini nifanye nini kuhusu jambo hilo? Naendelea tu, hivyo tu. Unaona? Na haina budi kupitia kwenye mfumo mwingine kabla ya mimi kama raia wa Marekani kulipwa pesa kwa cheki, haina budi kupitia kwenye kanisa hili, siwezi kulipwa pesa. Mnaona? Na hilo si sawa. Hilo linakiuka katiba. Lakini ni—nifanyeje juu ya jambo hilo? Hakuna kitu. Huyu mtoza ushuru hapa chini ndiye aliyeniambia nisingeweza kufanya hivyo, kwa hiyo, vema, hilo hapo. Kama ni hivyo, tufanye nini basi. Kwa hiyo, achana nao tu.

¹³ Nafikiri linapaswa kuwa ni jambo lile lile, kwamba ninii... kwamba ndugu zangu na dada zangu weusi huko Kusini hawapaswi kuwaasi ndugu zao na vitu kama hivyo juu ya kitu kidogo kama hicho. Jamani, inaleta tofauti gani kama ukienda shule *wapi* ama *nini*? Nilimwona mama mzuri mweusi asubuhi hiyo wakati walipokuwa... walikuwa na maasi huko Shreveport, na ilikuwa ni mzee mhudumu mweusi aliyeshikilia kuwaambia wanajeshi, alisema, “Naomba nizungumze nao.” Na kwa hiyo alikuwa ni mzee mcha Mungu, naye alisimama pale juu na kusema, “Kamwe sijapata kuionea aibu rangi yangu.” Akasema, “Muumba wangu alinifanya kile nilicho mimi, wala sijapata kukionea aibu, ila, hadi asubuhi ya leo.” Lakini akasema, “Ninapowaona ninyi, watu wangu, mkitenda jinsi hii,” kasema, “basi ninaona aibu kuwa mtu mweusi.” Kulikuwa na wanajeshi walioitwa, akapigiwa makelele akanyamaza.

¹⁴ Kwa hiyo mama mmoja mzuri mweusi, mwenye sura nzuri na elimu alisimama, mwenye akili, jamani, ya hali ya juu sana. Akasema, “Jambo la kwanza, sitaki watoto wangu wafundishwe na mwanamke wa kizungu.”

Kasema, “Kwa nini?”

¹⁵ Kasema, “Kwa sababu hatayajali maslahi ya watoto wangu ambayo nanii wangu... mwalimu mweusi atajali.” Kisha akasema, “Angalieni shule zetu huku. Mnapiga makelele ya nini?” Kasema, “Tuna vidimbwi vya kuogelea na kila kitu kwenye shule zetu, nao hawana vitu hivyo huko.” Kasema,

“Sasa, ninyi watu mnapiga makelele ya nini?” Nao wakamzomea akanyamaza, unaona.

¹⁶ Imevuviwa na kitu kibaya, mnaona, mnaona, hao, hao watu. Na hiyo ndiyo sababu ninasema jambo hilo, sio kwamba kuna ninii yoyote—unabii wowote kulihusu. Sina chochote juu yake kutoka kwa Bwana. Nanyi mwe na hakika sasa, kama nikisema jambo lolote kutoka kwa Bwana namna hiyo, kuwaambia, sikuzote ni... ninasema sasa. Bali Yeye anaponena, ninasema, “Si mimi, ni BWANA ASEMA HIVI.” Wala siwezi kulisema mpaka Yeye aniambie. Ninaweza kuwa nimekosea kabisa katika mawazo yangu juu ya Martin Luther King. Sijui, siwezi kusema. Hayo ni maoni yangu tu. Chochote kinachosababisha vurugu, hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa katika siku za mwisho. Na yote yamevuviwa na Shetani, kuvunjilia mbali jumuiya yetu na chochote tulicho nacho, chochote kinachoibuka namna hiyo. Kwa hiyo ninawaunga mkono watu hao huko chini, kamwe msifikiri siwaungi mkono. Ni—ninaunga mkono uhuru na kwa kila kitu, bali hao watu hawajadhibiti hali ya mambo sasa. Lakini yatakayofanya, ninaamini yataanzisha mapinduzi mengine kama mtu fulani hatayakomesha. Mnaona, ni Wakomunisti wakitenda kazi miongoni mwa watu hao.

¹⁷ Nilikuwa huko Afrika walipofanya jambo lile lile. Unaona? Nami ninajua Wakomunisti waliingia mle wakiwaambia hao watu weusi, “Loo, ninyi ni *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*. Ninyi ni *hivi*, *vile* ama *vinginevyo*.” Na muda si muda mwajua, ilisababisha maelfu yao kuuawa. Nao walifika wapi? Hakuna, mnaona, hakuna.

¹⁸ Nami na—naupenda uhai wa binadamu. Hebu na tumtumikie Bwana. Ufalme wetu ni wa huko Juu, hakuna kitu kuhusu kitu hiki hapa. Mradi tu tunakula, kunywa, na tunaweza kupata, unataka nini tena? Unaona? Kwa hiyo najua jinsi ingekuwa. Ni—ninatambua ya kwamba linasababisha tu vurugu.

Sasa, swali lingine lipo hapa.

Yohana Mbatizaji, wakati akikutana na Yesu, unaona, kwa nini Yeye akasema, “Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kutimiza haki zote”? Iliamaanisha nini?

¹⁹ Vema, ninamkumbuka Dr. Roy Davis, ra—ra—rafiki wangu msiri, aliyenibatiza wakati pekee niliopata kubatizwa. Naye alisema ya kwamba Yohana alikuwa anamaanisha, ninakumbuka jambo hili kwenye shule yao, alisema, “Yohana alijua ya kwamba kamwe hakuwa amebatizwa, yeye mwenyewe, kwa hiyo yeye... Yesu. Yohana alimruhusu Yesu ambatize.” Vema, hilo, ni—ninataofautiana na hu—huyo daktari mkuu hapo.

²⁰ Sio kwa ajili ya ubishi, bali kwa ajili ya Ukweli huenda nikasema jambo hili. La, hapo palikuwa na watu wawili,

viongozi wawili wa wakati huo, Masihi na nabii Wake walikutana majini. Sasa kumbukeni, Yohana alikuwa akibatiza, sio kwa ondoleo la dhambi, bali kwa toba. Sio kwa ondoleo la dhambi, maana dhabihu bado haikuwa imetolewa, mnaona, hapakuwepo na Dhabihu. Nayo hiyo Dhabihu ikamjia majini. Sasa angalia. Yohana alipoangalia juu na kumwona Yesu, yeye alisema, “Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe. Basi mbona unanijia mimi?”

²¹ Yesu akasema, “Kubali hivi sasa,” ambavyo ndivyo ilivyokuwa. “Kubali hivi sasa, kwa maana inatupasa, ama ni vema kwetu, kutimiza haki yote.” Ndipo Yohana, akiwa ni nabii ambaye hujiliwa na Neno la Bwana, humjia tu nabii. Yohana, akiwa ni nabii, alifahamu ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo Dhabihu. Na kulingana na Torati, kwamba dhabihu ilipaswa kusafishwa kabla haijatolewa, na hiyo ndiyo sababu yeye alimbatiza. Unaona? Yeye alisema, “Ndivyo itupasavyo kutimiza haki yote.” Dhabihu, ambayo ilikuwa ni Yeye, haina budi kusafishwa katika birika kubwa kabla haijatolewa kwa ajili ya dhabihu. Na Yesu alikuwa hiyo Dhabihu; na Yohana alijua hilo, naye alijua ya kwamba hana budi kuoshwa kabla ya kutolewa. Na basi mara baadaye, Yeye alitolewa kwa umma kwa ajili ya kule kujaribiwa na alikuwa ni Dhabihu kwa ajili ya wanadamu wote. Bwana awabariki.

²² Sasa tutakuwa na Ujumbe mdogo mfupi, na tunatumaini Bwana atatumalia baraka Zake. Sasa, labda, kama nikirudi... Ninaondoka juma hili lijalo kuwapeleka watoto katika likizo ndogo huko milimani. Na halafu kama niki—kama nikirudi kwa wakati, tunataka kuzungumza Jumapili ijayo asubuhi, kama inakubalika kwa Mungu na kwa mchungaji hapa. Tutawapasha habari zaidi juma hili, ninyi mlilo nje ya mji, kwa njia ya barua. Ninataka kuzungumza juu ya somo la ni kwa nini hasa tunaamini mambo ambayo tunaamini kumhusu Kristo, ni kwa nini inabidi iwe ni njia hii wala haiwezi kuwa njia nyingine yoyote. Unaona? Na kulithibitisha kwa Maandiko. Sasa, Bwana akipenda. Nisipofanya hivyo, nitajaribu kuwaona kwenye msimu huu wa baridi kali ama msimu ujao wa kiangazi, mojawapo, tutakaporudi, Bwana akikawia. Tunarudi sasa nyumbani Arizona, kusudi tukawapeleke watoto shuleni.

²³ Sasa, asubuhi ya leo, kabla tu ya maombi kwa ajili ya wagonjwa, tutasoma baadhi ya Neno la Mungu. Ambalo, tunajua ya kwamba bila ya Neno hili, haiwezekani, hakuna kitu kinachoweza kufanyika. Na Neno tu ndilo linaloweza kuleta baraka hizi ambazo tunaomba kwa ajili ya wagonjwa na wahitaji. Nami ninataka kusoma baadhi sasa kutoka kwenye Petro wa Kwanza, mlango wa 5, kuanzia kifungu cha 1. Na halafu kutoka kwenye Kitabu cha Waebrania, nataka kusoma Waebrania 2:2-4.

Nawasihi wazee walio kweni, mimi, niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa kuteswa kwa Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye.

Lichungeni kundi la Mungu lililo kweni, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo.

Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi.

Na mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka.

Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee. Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; wala msijifunge... pia jifungeni unyenyekevu: kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.

Basi nyenyekeeni... chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake.

Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.

- ²⁴ Na katika Waebrania, mlango wa 2, tunasoma Maneno haya. Sasa ninavuta kwa ajili ya kutoa fungu la maneno, “kumtwika fadhaa zenu.” Ninaninii... Somo langu ni: *Yeye Hujali. Je! Wewe Unajali?* Ninataka kusoma sehemu hii sasa, wakati mkifungua Waebrania 2, mpate kuona ma—maana halisi ya Maneno haya, kile hayo, kile fungu hili la maneno linachomaanisha.

Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa.

Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika yalikuwa—lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki,

Sisi je! tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia;

Mungu... naye akishuhudu pamoja... kwa ishara na... ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe.

- ²⁵ Ninataka kutumia somo hapa, la, “Yeye hujali.” Na, “Nawe Je?” Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye aliwajali watu. Wazo lake linaibuka niani mwangu kabla tu ya kuzungumza au kuwaombea wagonjwa, bila kujua tutakuwa na mstari wa maombi wa—wa namna gani.

- ²⁶ Kwanza, na kulikaribia hili, wasikilizaji hawana budi kutiwa mafuta kwa imani. Wewe, kama huna imani, basi

hakuna—hakuna hata haja ya kuja kuombewa, kwa maana itahitaji imani yako na imani yangu pamoja; imani yangu kumwamini Yeye, imani yako kumwamini Yeye. Kwa hiyo tusisahau jambo hili sasa ninapoendelea mbele. Inatupasa kuwa na kitu fulani kwa dhahiri, pamoja na ushahidi, namaanisha, kwamba tunaweza kuwekea msingi imani yetu juu ya yale tunayojaribu kufanya. Maana kama mtu akikaribia chochote anachotaka kufanya, pasipo imani ya kutosha, hana budi kushindwa. Lakini kama anaweza kukikaribia kwa imani ya kutosha, basi hana budi kufanikiwa kama ni kulingana na mapenzi na kusudi la Mungu kufanya hivyo.

²⁷ Sasa, nilikuwa nikifikiri juu ya Yeye kujali. Jana jioni, kwa namna fulani, kiajabu, niliongozwa na Roho Mtakatifu. Wakati nilipokuwa nikiwangojea jamaa fulani waje wamsaidie Ndugu Wood kuweka tre—trela ambalo alikuwa ameunda nyuma ya gari lake. Sikujua ni kwa nini nilikuwa nikijaribu kumtafuta rafiki yangu mwema, Ndugu Evans, nami nikaenda, nikaanza kupanda barabara kuu. Jambo ambalo, mke wangu na familia wanaoketi hapa nyuma wanajua ni kweli. Na kwa namna fulani, kiajabu, niligeuka nikarudi mahali fulani, moteli moja.

²⁸ Na, loo, jinsi ilivyofurahisha moyo wangu kuwaona wengi wa marafiki wangu wamekusanyika pale katika muda wa dakika mbili hivi, mpaka ikaifunga njia, magari yasingeweza kupita tena, marafiki halisi kweli, wakiendesha magari umbali wa mamia ya maili, kutoka Georgia na Tennessee na Alabama, na kila mahali, ili tu ku—kusikia ibada. Ndipo wazo hilo likaja moyoni mwangu, “Basi inanipasa kuwaambia nini watu hao, nikijua ya kwamba kwenye Siku ya Hukumu itanibidi kujibu kwa ajili ya yale ninayowaambia?” Nami pia ni—ni mpenzi wa maisha haya mazuri sana yajayo, nami ni—ninataka kuwa kule.

²⁹ Halafu kwa jinsi ya ajabu nilienda mahali ambapo niligeuka isivyo kawaida. Badala ya kugeukia pale, nilipanda kwenda kugeuka. Taa zikawamulika mume na mke wazuri sana wakiwa nje, wasichana wawili wazuri ambao nilikuwa tu nimewaoza kwa wahudumu vijana wawili wazuri. Na Shetani, baada ya kumwona m—mhudumu, mmoja wao huduma yake ikiwa imeanza naye akachukua m—mwenzi wa maisha papa hapa, madhabahu hii. Waliondoka wakaenda kwa furaha kwenye fungate yao, ndipo—ndipo adui akamrukia kijana mwanamume huyu. Nami ninasema hili kuelezea yale ninayosema, “Je! Yeye Hujali?” Kwa namna fulani, wakiwa na imani isiyoweza kusema “la,” walirudi na kurejea huku, wakijua baada ya kuwa huko kote (huko mbali mashariki) hapa mahali fulani kwenye fungate yao, wakarudi nao walikuwa wameketi, wakingojea. Nami nikaingia, kijana mwanamume mzuri mwenye sura nzuri; mke wake ameketi nje, akilia, yeye pamoja na maskini mwenzi wake. Na mtu huyo mwingine na ndugu huyo mwingine wakija,

wakikimbia, ambaye ni rafiki wa kijana mwanamume huyu, wakisema, “Loo, Ndugu Branham, *hivi na vile* vimetukia.”

³⁰ Nikaenda pale na kumwona kijana mwanamume huyu mwenye sura nzuri ameketi pale, kwenye kilele kabisa cha maisha yake, kiongozi wa vijana wa kiume, ameketi pale, naye Shetani amemfunga. Kamwe hakuona, bali nilichukua mkono wangu (wa kushoto) kupeana mikono na mkono wake (wa kuume), kuona kama ugonjwa fulani ulikuwa umemshika. Lakini hakukuwa na ishara ya mtetemeko. Nikitoka moja kwa moja kutoka chumbani nilikokuwa nikiomba na kufunga, na kumngojea Bwana, upako wa Roho Mtakatifu ulikuwapo, na hiyo ndiyo sababu alituongoza, mnaona. Halafu nikiona kivuli hiki cha giza juu yake. Kamwe sikusema nilichokuwa nikifanya. Lakini muda si muda yote yalikuwa yamekwisha, ubaridi wa mikono yake ulikuwa umeondoka, alikuwa akipaza sauti na kumsifu Mungu, dakika chache akiisha jirudia. Nao hawa hapa wameketi papa hapa asubuhi ya leo, wameketi miongoni mwa wasikilizaji. Mnaona jinsi Shetani alivyokuwa akijaribu kumtibu huyo kijana mwanamume, akimrejesha kwenye kinyongo fulani kitakachoumbwa, ambacho Roho Mtakatifu alijua, nami nilikiona kwa ono la Bwana. Lakini Mungu alimjali mtu huyo. Mungu alimjali mvulana huyo mdogo.

³¹ Nikiingia tu dakika chache zilizopita, ma—mama mmoja, nilimwona ameketi hapa kwenye marefu, bila ninii. . . alikuwa tu amepata kiti kwa namna fulani, na akaketi chini. Akasema, “Miaka tisa, Ndugu Branham, nimejaribu kukupata.” Naye akasema, “Nimekata tamaa kabisa! Nilikuja hapa nimechelewa, wala hata nisingeweza kupata kadi ya maombi nipate kuwa kwenye mstari wa maombi.”

³² Billy, bila shaka, ni jukumu lake kuhakikisha ya kwamba sisumbuliwi, huniingiza na kunitoa. Msimchukie Billy, ameamriwa na halmashauri hii ya wadhamini kufanya hivyo. Na kama hakufanya hivyo, nisingeweza kufika kwenye mstari wa maombi, kuingia hapa ndani. Mnatambua hilo. Mnaona, hapana budi pawe na mfumo kwa chochote tunachofanya. Sisi—hatuna budi kuwa nao, mnaona. Lakini yeye akisema, “Njoo, baba, harakisha,” hili.

³³ Mama huyo akarudi nyuma. Naye akasema, “Ndugu Branham, neno moja tu nawe.” Nikisimama pale, ono lilitokea juu ya mwanamke huyu mdogo mwenye sura nzuri, ndipo nikaona moyo wake ulikuwa umelemewa. Naye alikuwa akijaribu kufanya kazi apate riziki. Ndipo ja—jambo kubwa likatukia huko nyuma, huko nyuma kabisa katika wakati wa wazazi wake, ambalo lilisababisha jambo hili kuu kumpata, Naye Bwana Yesu akalifunua na kuonyesha kwamba lilikuwa ni nini. Na hapo, katika dakika moja, akaliondoa kwa mwanamke huyo. Akaenda kote akishangilia. Na sasa ameketi hapa katika wasikilizaji pamoja nasi sasa, akishangilia, kwa machozi, kama

vile anavyoyapangusa macho yake sasa, akijua ya kwamba ukweli wa jambo hilo ulijulikana. Na hicho, ambacho, maskini mwanamke huyo mwenye fadhaa, ambaye alikuwa na wasiwasi sana hakujua la kufanya na nafsi yake, na akifikiri ya kwamba alikuwa amekwisha, wala hapakuwapo na Roho Mtakatifu, na hii ndiyo siku yake ya mwisho. Alikuwa amejaribu kwa muda wa miaka tisa naye alikuwa karibu kufikia mwisho wa kukata tamaa. Mungu alimjali maskini mwanamke huyo ambaye hakuna anayemjali. Mnaona? Ni wakati wa jinsi gani! Yeye hujali.

³⁴ Wakati alipokuwa hapa duniani, kama ninavyosema, Yeye aliwajali watu sana hata akawaponya wagonjwa wao, akaifariji moyo yao, akawaambia kuhusu ma—mahali ambapo Yeye angeenda na kuwaandalia, kisha arudi tena kuwapokea Kwake. Aliwajali. Na hebu angalia, Yeye alijali sana mpaka, wakati alipojua ya kwamba hana budi kuondoka kusudi atulettee kitu hiki kikubwa, Yeye alisema, “Sitawaacha ukiwa, bali nitamtuma Roho Mtakatifu, Naye ataendeleza fadhili Zangu kwenu,” mpaka Yeye atakaporudi. Hakuna mtu anayejali kama Yesu. Tukijua ya kwamba mwili Wake, kama Kuhani Mkuu, katika kazi ya uombezi anayofanya sasa, Mwili huo hauna budi kuwa Mbele za Mungu wakati wote, kwa ajili ya uombezi, ili kwamba Mungu asiweze kuiona dhambi ya mwenye dhambi; Yeye anaona tu Damu ya Mwanawe. Na tukijua ya kwamba, Yeye alimtuma Roho Mtakatifu arudi aendeleo kuwafariji watu Wake. Je! Yeye anajali? Hakika, Yeye anajali. Sasa, alikuwa aendeleo kuwajali watu Wake, watu Wake hapa duniani, kwa jinsi ile ile aliyowajali wakati alipokuwa hapa. Kwa sababu alisema katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 15, kama mkitaka kufanya... Nina mihtasari iliyo hapa pamoja na Maandiko ambayo ninarejea, Yohana Mtakatifu 15:26 na 27.

³⁵ Ninawaona wengi wenu mkiandika Maandiko. Kwa hiyo huenda nikarejea kwa hili kama hamliui, mara nyingi, kwenye Maandiko. Mimi huandika Maandiko, ndipo ninajua ninalonena habari zake kutoka hapa, maana daima yako kwenye Neno la Bwana. Mnaona?

³⁶ Yeye alisema, akiisha kuja Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma katika Jina Lake, angemshuhudia Yeye. Kwa maneno mengine, angefanya jambo lile lile alilofanya Yeye. Roho Mtakatifu akitenda kazi kupitia maskani aliyokuwa ameitakasa, angefanya jambo lile lile alilofanya. Sasa, jinsi hilo linapaswa kutufanyia! Ndipo tunajua ya kwamba moja kwa moja miongoni mwetu leo tunaye Bwana Yesu yeye yule anayefariji katika umbo la Roho Mtakatifu, ofisi nyingine ambayo Mungu Mwenyewe anafanyia kazi.

³⁷ Yeye alikuwa ni Faraja kwa Israeli wakati wangeangalia juu na kuona ile Nguzo ya Moto, na kumsikia nabii akinena Maneno

yaliyokuwa ni kweli, na Mungu akiyathibitisha. Hiyo ilikuwa ndiyo Faraja yao.

³⁸ Yeye alikuwa ni Faraja wakati alipokuwa hapa duniani kama mwanadamu, Mungu aliyefanyika mwili. Mungu akijiwakilisha Mwenyewe na kujionyesha Mwenyewe kupitia kwa Mwa—Mwanadamu, Kristo Yesu, ambaye aliahidi ya kwamba “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Nami ninaenda kwa Baba, na nitamtuma Roho Mtakatifu, ambaye atakuwa ni Mimi katika umbo la Roho. Nami nitakuwa pamoja nanyi, na kukaa ndani yenu. Na mambo yale yale ambayo nimefanya hapa, Roho Mtakatifu atafanya tena katika Jina Langu, atakapokuja.” Unaona? Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Kusema neno dhidi ya Huyu” sasa baada ya ule upatanisho tayari kufanywa, ilikuwa ni dhambi isiyosamehewa, “kumkufuru Roho Mtakatifu.”

³⁹ Naye angefanya hivyo kwa njia ile ile, kusudi tujue kama ilikuwa ni faraja kutoka kwenye mwelekeo fulani wa ulimwengu, kama tungejua endapo ilikuwa ni faraja kutoka kwa mzee ambaye angetutupia mikono na kutukumbatia kidogo na kutufanya tujisikie vizuri, ama—ama neno fulani la kitheolojia la dhehebu ambalo lingesema “sasa wewe ni mali yetu, nasi tunalo; wala usiwe mfuasi wa hayo mengine, maana hawana.”

⁴⁰ Alilihakikisha hili moja kwa moja, unaona, “Yeye atanena kwa Jina Langu. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, wakati Yeye akiwa juu yenu.” Unaona, Yeye angefariji kwa njia ile ile, kwa kuzisamehe dhambi zetu zote, kuyaponya magonjwa yetu yote, na kusema nasi juu ya faraja ya Ufalme ujao. Unaona, akijithibitisha Mwenyewe miongoni mwetu, kama vile Mungu alivyojithibitisha Mwenyewe miongoni mwetu kwa Yesu Kristo. Na katika—katika II Timotheo . . . I Timotheo 3:16, imeandikwa hivi, kumjua Mungu, “Bila shaka tunatambua ya kwamba siri ya utauwa ni kuu, kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili.” Tulimwona Mungu katika mwili. Hiyo ilikuwa ni faraja ya Mungu, kujua ya kwamba alikuja sana (Yeye alitujali) hata akawa mmoja wetu. Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Sio mtu mwingine tu, bali ni Mungu Mwenyewe!

⁴¹ Na sasa kuifanya hatua nyingine moja karibu zaidi, Yeye anamtuma Roho Mtakatifu kushughulikia faraja zetu, na Yeye anakaa *ndani* yetu. Loo, Yeye kweli hujali!

⁴² Sasa hatuna budi kuiendea sehemu nyingine ya Maandiko hapa, ama wazo lingine kuunga hili mkono. Kabla sijaondoka, huenda nikasema jambo hili: kila mtu hana Mfariji huyu. Wao, wao hawana, hawana Huyu. Kwa hiyo sababu ya wao kutokuwa Naye, ni kwa sababu hawamkubali. Ni kwa ajili yao, bali hawamkubali. Sasa, ninatumaini ya kwamba ninyi ni wa kiroho vya kutosha ku—kusoma yale ninayosema. Mnaona? Ninalizungumzia kundi la watu watakaombewa katika dakika chache. Nasi tuna faraja hii katika Roho Mtakatifu ambaye ametumwa kuwa Mfariji, bali watu wote hawatampokea Huyu.

Hawamwamini. Mnaona? Wao, kusudi wafanye jambo hilo, basi wanakusanya faraja yao kutoka mahali pengine, njia zingine. Kama hawamkubali Mfariji aliyetolewa na Mungu, basi hawana budi kupata mfariji mwingine, unaona, kwa kuwa huwezi kuishi bila ya kitu cha kukiishia.

⁴³ Nami ninatumaini ya kwamba kila mmoja wenu atapata jambo hilo, hasa sana ninyi watu mtakaombewa, ambao hamna faraja asubuhi ya leo, pengine mkiwa na shida ambazo madaktari hawawezi kuzigusa.

⁴⁴ Nasi tunaamini ya kwamba madaktari huwasaidia watu. Ninaamini ya kwamba Mungu huponya kwa dawa. Mungu huponya kwa upasuaji. Mungu huponya kwa kuhurumiana. Mungu huponya kwa upendo. Upendo kidogo tu huenda umbali mkubwa. Hebu mtu awe amefadhaika sana, na hebu uwaonyeshe unawajali. Unaona? Mungu huponya kwa upendo. Mungu huponya kwa maombi. Mungu huponya kwa miujiza. Mungu huponya kwa Neno Lake. Mungu huponya! Hata chanzo chake kiwe ni kipi, Mungu huponya kwa hicho. Mungu Ndiye aponyaye, kwa kuwa Yeye alisema, “Mimi ni Bwana akuponyaye magonjwa yako yote.” Kwa hiyo yote yanapaswa kutenda kazi pamoja, na watu katika huduma mbalimbali wanapaswa kufanya kazi pamoja kwa ajili ya jambo hilo. Unaona? Sasa, bali hawafanyi hivyo, kwa sababu wakati mwingine wanakatazwa kuchukua misimamo fulani juu ya Neno la Mungu, kwa sababu madhehebu yao fulani hayawaruhusu kufanya hivyo. Bali hilo haliizuii ile Kweli, ni vile vile tu, Mungu anaendelea kuponya vivyo hivyo.

⁴⁵ Kwa hiyo wanajaribu kupata faraja kutoka mahali pengine. Hebu na tuzungumze kwanza juu ya nafsi.

⁴⁶ Tunaona ya kwamba watu wengi wanajaribu kupata faraja kwa kunywa pombe. Mwajua, tuna msembo ambao unajulikana sana miongoni mwetu siku hizi, ya kwamba—ya kwamba wahudumu wengi wakati mwingine hunywa pombe kabla ya kwenda mimbarani, wanakunywa pombe nyi—nyi—nyingi zenye kileo. Imejulikana wahudumu wanaonekana jukwaani, ambao hata huyumbayumba chini ya nguvu za pombe. Na hilo—hilo halipaswi kuwa. Halipaswi kuwa. Ni kwa sababu mara nyingi huenda tukamlaumu mtu huyo wakati pengine haitupasi kufanya hivyo, tunapaswa kutafuta kujua shida ni nini. Wengi wao waliongolewa kutoka kwenye pombe. Na tunaona, kama wako katika hali hiyo, ni fedheha na ni lawama. Lakini si lawama zaidi ya vile ingekuwa kudanganya, kuiba, ama kuwatamani wanawake, ama kitu kingine chochote kilicho kwenye zile amri. Unaona? Na labda mtu amezaliwa mwenye tamaa kali, naye anawaona hawa wavua nguo mamboleo mtaani, na yeye—yeye daima yuko katika shida. Unaona? Yeye, huyo, mtu huyo amezaliwa namna hivyo. Sasa, kile anachopaswa kufanya,

mhudumu anayekunywa pombe, ama nanii—ama mwanamke anayevuta sigara ama ambaye...

⁴⁷ Anavaa kizinifu, akijaribu kupata faraja yake kutokana na kujipamba kwelikweli, hata anataka kumfanya mwanamume kumwangua. Hakuna sababu nyingine. Yeye ni nusu kichaa. Unaona? Hakuna mwanamke mwenye akili timamu angewazia kujivua nguo mbele ya mwanamume, aliye na akili timamu. Unaona? Hakuna sababu ya jambo hilo hata kidogo. Naye, bali anajaribu kuninii, wasichana hawa wadogo siku hizi wanaoenda mitaani, wao ni ninii hasa... Vema, samahani kwa tamshi hilo. Pia kumbukeni, kanda hii haiendi tu kwa watu hawa hapa, inaenda kote ulimwenguni. Unaona?

⁴⁸ Na mwa—mwanamke ambaye angevua nguo zake, kwa kuwa anajua kuna joto zaidi. Atembee huko nje kwenye jua, uchi, halafu atoke akiwa amevaa nguo, basi ipi iliyo na baridi zaidi? Wahindi huko chini katika Papagos na Navajos; Wapapagos, hasa, na wa ile hifadhi, hao wanawake wanatoka wakiwa wamejifunika mablanketi mazito ya kitani, na kuketi huko nje kwenye jua wapate kupoa. Kwa nini? Wanatoa jasho, na upepo unaovuma unafanya kiyoyozi, mnaona. Nao hawa wanawake hawana sababu nyingine yoyote ila tu... Hawajui hilo, hawalitambui. Sisemi kwamba wanajua. Wengi wao ni wanawake wazuri, wala sisemi jambo hilo kwa ujuvu. Ninalisema ku—kujaribu ku—ku—kuwaamsha. Mnaona?

⁴⁹ Ni Shetani tu, unaona. Mnatambua jinsia hiyo nyingine, jinsia ya kiume inapoangalia kitu kama hicho, inawapa ashiki sana hivi kwamba wata—wataalika tairi zao na kupiga mbinja wa—wa—wa mbwa mwitu. Na—na—nao wanafanya jambo hilo kwa nini? Mwanamke anafanya hivyo kusudi amfanye mwanamume kufanya jambo hilo. Ni kwa nini unatoka, moja kwa moja kwenye joto kali la mchana, na saa kumi alasiri, kukata nyasi wakati watu wanapotoka kazini mwao na vitu kama hivyo? Inaonyesha ni roho ya wenda wazimu. Nami ninajua wengi wao wanaweza kuwa na kiwango cha akili ya juu kwa mamilioni ya maili kuliko yangu, bali mimi ninapima kiwango cha akili yako kwa Neno la Mungu na kuona mahali inakotokea. Mnaona? Hicho ni kiwango cha akili cha kisasa, bali ushuhuda wenyewe wa matunda ya maisha unathibitisha. Kwa hiyo wanajaribu kupata faraja kwa jambo hilo.

⁵⁰ Wengi wao husema, “Vema, sifanyi jambo hilo.” Lakini mtu wanajivalisha wenyewe kwa kutamanisha sana hata wanajaribu kuwa wa kisasa zaidi kuliko mwanamke atakayeketi karibu nao kanisani kesho yake asubuhi, kuvaa kofia bora zaidi ama nguo bora zaidi, kwa kuwa mnaweza kuzigharimia. Mnaona? Mnaona, dhambi inafikia huko chini kabisa. Nao wanajaribu kupata faraja kwa kufanya jambo hilo. Nao wanainii...

⁵¹ Limekuwa ni jambo ambalo hata limeipiga kabisa nchi nzima, sio tu nchi nzima, bali ulimwengu mzima. Ningesema

mambo mengi hapa, lakini, kuokoa wakati, ibada ya uponyaji inakuja, mimi—mimi ningeweza kuzungumzia jambo hili kirefu, bali sitalizungumzia. Nina hakika mtafahamu ninalomaanisha. Hili, limeuvamia ulimwengu wa kisiasa, maisha ya kisiasa, maisha ya jamii, maisha ya uadilifu wa taifa, ya watu kote ulimwenguni. Imefikia mahali ambapo mtu anataka kuwa mwanasiasa kwa ajili tu ya jina la kuwa mwanasiasa. Wana fedha nyingi sana, wanaweza kuzivutia kura na kukodi mitambo ya kufanya hivyo, na—na kadhalika, kwa ajili tu ya jina, na kugharimu mamilioni na mamilioni ya dola, unaona, kwa ajili tu ya jina la kuwa mwanasiasa mkuu. Yamesemwa ya kutosha kuhusu jambo hilo, mnajua kile ninachomaanisha.

⁵² Na maisha ya jamii! Watu wanajaribu kukusanyika pamoja katika maisha haya ya wendawazimu ya kijamii. Msiniambie ya kwamba ulimwengu haujaingia kichaa, na ukifanya jinsi unavyofanya. Hakika una kichaa. Hakika. Ni ulimwengu wenye fadhaa. Na kwa neema ya Mungu ndiyo njia tu tutakayoepukana nao. Angalieni, katika maisha haya ya jamii, watu wamefikia mahali ambapo wao—wao wanajumuika pamoja katika makundi madogo, nao wanaingia mle na kuwaza, “Sisi ni bora kuliko kundi hilo lingine.” Unaona? Na hiyo, hiyo inafanywa tu namna hiyo. Na ni uadilifu, limeshambulia uadilifu wa watu mpaka, kusema kweli, enyi marafiki, hata siamini ya kwamba (walimwengu) neno “uadilifu” linatambulika miongoni mwa asilimia tisini ya watu wa taifa hili. Hata hawajui kile (walimwengu) neno “uadilifu” linachomaanisha. Lime—limewapotelea. Nalo limefanya hivyo kwa ujanja sana.

⁵³ Shetani ni mjanja sana, unaona, naye anafanya jambo hilo kwa urahisi sana, m—mjanja sana, kidogo tu *hapa* na kidogo *pale*, na kuliachilia. Ana wakati mwingi sana, kwa hiyo yeye huingia tu kidogo *hapa* na kidogo *pale* na, muda si muda mwajua, polepole watu wanaingizwa ndani yake. Ingalikuwaje kwa mwanamke, huko nyuma wakati nilipokuwa mvulana mwenye umri wa miaka kumi na sita, kama angalitembea mtaani kama anavyofanya siku hizi katika mtindo huu wa kujivua nguo? Mbona, wanalimfunga gereza. Vema, kama ilikuwa ni kosa wakati huo, ni kosa sasa. Unaona? Lakini, unaona, Shetani alianza tu kukata sketi zao, na kuzifupisha, na—na itakuwa ya kwamba mtu fulani atabuni moja fupi kidogo kuliko mikini ama bikini, ama vyovyote mnavyokiita kitu hicho, kufikia kwenye jani la mtini. Ninyi kumbukeni! Hiyo ni kweli, itarudi moja kwa moja kama ilivyokuwa kule nyuma. Na iko, kwa kweli iko sasa.

⁵⁴ Na sasa tunaona, mambo hayo yote ni kwa sababu watu wanajaribu kupata faraja. Wanajaribu kupata kitu ambacho wao... Pia kumbukeni, faraja yako ndiyo dini yako, nawe unayafanya mambo hayo dini yako. Unaona? Ni huzuni jinsi gani katika kutambua ya kwamba mauti imewekwa papo hapo mbele zako. Unaona? Mpaka, yote haya yametokea hata inaonekana

kana kwamba hakuna m—msingi imara uliosalia nchini wa kujengea kitu chochote juu yake.

⁵⁵ Hebu niwaulize tu jambo fulani. Huwezi mtu kuamini chochote, ni vigumu, ili Biblia. Tungali tuna Kristo; Mungu ashukuriwe. Unaona? Hu—huwezi kuamini chochote. Unaingia kwenye. . . Kwa mfano, unapoifungulia televisheni yako (ninyi mlio na vitu kama hivyo), na wakati unapoifungua televisheni yako na kuona ma—matangazo ya biashara, vema, kama mtu alijaribu kuishi kwa sehemu moja ya mia ya hayo matangazo ya biashara, mtu ungekufa katika muda wa juma moja. Unaona, usingeweza kuishi kwayo. Na kitu chenyewe ambacho kampuni fulani itakielezea, kama bidhaa, na kusema, “Kitu ndicho *hiki* hapa, wala usichukue *hiki* hapa,” na kampuni iyo hiyo ndiyo inayouza bidhaa hiyo. Ndipo tangazo lingine litaingia, liichukue *hii* upande huu wala si *ile*, na ni kampuni ile ile. Wamarekani wanashawishika kwa upuuzi kama huo, mpaka kitu hicho chote kimeoza, mpaka hakuna matumaini yoyote. Hakuna mtu anayejua la kuamini. Lakini nitawaambieni baada ya kitambo kidogo kitu cha kuamini, kama mkitaka faraja, Bwana akipenda.

⁵⁶ Watu, wanadanganya, wanahadaa, wanaiba, mpaka karibu inakulazimu kuweka dhamana upate kumkopa mtu dola tano. Ni ninii. . . Mwajua, Biblia inazungumzia hilo, ya kwamba hakutakuwako na upendo katika siku za mwisho ila tu miongoni mwa wateule. Hiyo ni kweli. Maandiko yanazungumzia hayo, kwamba mume atamchukia mkewe, na mke angemchukia mumewe, watoto watawachukia wazazi wao. Ni miongoni tu mwa Wateule wa Bwana ambapo patasalia upendo wowote.

⁵⁷ Makanisa yameingia kwenye kitu kile kile kutokana na maisha ya jamii. Waliingiza kanisani, maisha yao ya jamii na siasa zao na vitu vyao vingine, mpaka wamelichanganyisha kanisa sana hata halijui la kufanya. Waliingiza siasa kanisani. Waliingiza pia maisha ya jamii, maisha yao ya jamii kanisani, shughuli zao za jamii, bingo au banko, ama chochote wanachokiita, na vyakula hivi vya jioni na madansi, na kadhalika, katika nyumba ya Bwana. Kwa nini, ni—ni masikitiko.

Wao wanasema, “Vema, sasa, hiyo si ninii, hiyo ni kwenye jengo la kando.”

⁵⁸ Kumbukeni, ilikuwa ni kwenye jengo la kando ambapo Yesu aliwapiga mijeledi na kuwafukuza wa—wafanyabiashara pamoja na bidhaa zao, na akasema, “Imeandikwa, ‘Nyumba ya Baba Yangu imefanywa nyumba ya Sala,’ nanyi mmeifanya pango la wanyang’anyi.” Unaona? Si halali, sijali liko wapi. Mradi tu kanisa. . . Kanisa sana sana si jengo, ni watu walio humo jengoni. Na kama watu hao wanashiriki katika jambo hili, mbona, si halali. Nao wameleta desturi hiyo.

⁵⁹ Sasa tunaona ya kwamba makanisa, pia, daima yanaahidi kitu fulani, kama inavyofanya televisheni na kadhalika, ambapo kamwe hawafikii kwenye kitu—kitu walichoahidi. Kama ambavyo nimesema mara nyingi, nukuu ya kale, “Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, anamsifu Mungu kwa yale atakayofanya (akitazamia yale atakayofanya), na halafu anapuuza yale Yeye anayofanya.” Unaona, wao—wao—wao wanashindwa. Na hivyo ndivyo yanavyokuwa ni historia baada ya kitambo kidogo, ya machafuko, mnaona, kwa sababu wanashindwa kutambua sasa! Mtu unaweza kuzungumza juu ya faraja iliyotolewa na Kristo wakati mmoja, na kusema atatoa faraja fulani katika nyakati zijazo, lakini ukatae faraja uliyo nayo hapa sasa kwa ajili yako. Unaona? Tunaona liko kwenye msingi ule ule. Vema, limekuwa ni jambo kubwa. Sasa tunaona ya kwamba wao—wao wanakuja. . .

⁶⁰ Hayo hata yameingia katika Pentekoste, katika makanisa. Yameingia kwenye milki za Kipentekoste, kwamba daima wanaahidi kitu ambacho kamwe hawakifikii. Imetokea kwamba kila jamaa ana mhemko tofauti, na—na anaupata kama ni wa Kimaandiko ama sivyoyote, nao wanaahidi kitu ambacho kamwe hawakifikii, mpaka inaonekana kana kwamba imefikia mahali haonekani kana kwamba kuna uaminifu wowote. Wa—watu hawafikii kwenye kile kiini halisi cha uaminifu. Limepoteza ninii. . . Neno lenyewe la Kiingereza *uaminifu* limepoteza thamani ya—yake kwa watu. Ama, kwa maisha ya—ya watu, imepoteza uaminifu kwao. Sasa inaonekana hawaelewi.

⁶¹ Hata kwa maungamo yetu! Sasa, ninawatakeni ninyi watu mnaokuja, ama mlio hapa na mnashikilia. . . ama kwenye ninii—kwenye kanda, ninawatakeni msikilize nukuu hii kwa makini sasa kwa dakika moja. Ni—ni. . .

⁶² Isipokuwa uwe ni mwaminifu kabisa! Na huwezi kuwa mwaminifu mpaka utakapoelewa vizuri kabisa. Kama unadhania, ama kukisia, ama kutumainia ni hivyo, basi haiwezekani kuwapo na vilindi vya uaminifu ambavyo Mungu anahitaji. Yenyewe, imani, si “natumaini ndivyo ilivyo” ama “inaweza ikawa ni kweli.” Haina budi kuwa kabisa ni “Amina!” Ndio mkataa wako. Ni—ni—ni niniii yako—ni yakini yako. Ndicho kitu ulichofungiwa kwake. Unaona? Huna budi kufikia kwenye mkataa wako, ya kwamba “Ni Kweli na kuna. . . Si kitu ila ni kweli, na haina budi kuwa hivyo!” Na halafu unapojua hilo moyoni mwako, ndipo huna budi kuikaribia kwa maisha yako yote, nafsi, mwili, yote yaliyo ndani yako, uuze tu kabisa kila kitu kwa ajili yake. Kama vile Yesu alivyotufundisha kwa fadhili katika yule mtu aliyenunua lulu, naye akapata Moja ya thamani kuu naye akauza zingine zote zake apate kuifikia Hiyo. Kweli zote na kila kitu alichokuwa nacho, ingawa zilikuwa ni lulu nzuri, yeye—yeye. . . hii Moja ilimaanisha yote kwake.

Na unapoupata Mkataa wa Mungu, Neno Lake, ahadi juu ya jambo fulani, inakubidi kujua kwanza ya kwamba ni Neno la Mungu, ya kwamba jambo unaloliona likitekelezwa ni Mungu. Ha—hakuna—hakuna “huenda ikawa ndivyo, ingewezekana, inaonekana kana kwamba huenda ikawa.” “Ni Mungu!” Ndipo unapofikia mahali hapo, basi hiyo ndiyo ile Lulu ya thamani kubwa, huna budi kuachana na chochote mtu yeyote anachokwambia kinyume Chake. Haikupasi kuangalia kile mwanadamu ametimiza. Huna budi kuangalia kile Mungu amesema na kile Yeye ameahidi, na kumwona Yeye akikifanya, ndipo huo ndio Mkataa wako papo hapo. Halafu basi kila kitu ulicho wewe, kila kitu ulichokuwa, kila kitu unachotumaini kuwa, hakina budi kuwekwa juu ya Hili kana kwamba tu ilikuwa ni mauti na uzima kwako kwenye wakati huo.

⁶³ Ninafikiri jambo moja linalowazuia watu wetu kuponywa ni ukosefu wa toba, ni ukosefu wa maungamo ya kweli. Sasa, kwa mfano, hili linaweza likasikika kidogo ni baya, bali silimaanishi hivi. Lakini, nikimwangalia mke wangu ameketi hapa. Kama ningetoka hapa leo na kumkumbatia mwanamke fulani na—na kufanya mapenzi naye, na ningejua wakati huo, baada ya kufanya hivyo, ya kwamba nilikosea, vibaya sana. Sasa, bila shaka, Mfariji wangu angenizuia kufanya jambo hilo. Unaona? Unaona? Lakini ninamaanisha kama mimi—kama nilifanya hivyo, nami... ilitokea kwamba nililifanya ama jambo lolote kama hilo. Halafu ninajua jambo la kwanza ni kumwambia mke wangu, kabla sijaweza kumwambia Mungu, “nisamehe,” maana nilitenda dhambi dhidi yake. Kama ukija madhabahuni na ukumbuke una jambo fulani, nenda kanyoshe hilo kwanza, kabla hujatoa sadaka yako. Kwa hiyo inanibidi kwenda kwake. Ninaamini kuungama ni kunyosha mambo pia. Si maungamo ya kweli isipokuwa mambo yamenyoosha.

⁶⁴ Vipi kama nilisema sasa, “Nitaungama hilo, kwamba nilikosea, niseme, ‘Bwana Mwema, Ee Rafiki yangu, unajua ya kwamba ninakujua vizuri sana. Mungu asifiwe! Haleluya! Mimi—mimi—mimi—mimi nafikiri Wewe ni Jamaa mzuri wa siku nyingi. Nisamehe. Unajua, Rafiki yangu, wa zamani sana, mimi—sikumaanisha jambo hilo hivyo’”? Unaona?

⁶⁵ Sasa, unasema, “Huko ni kukufuru.” Naam. Kufanya maungamo kama hayo, ni kukufuru.

⁶⁶ Lakini vipi kama nikienda niseme, “Bwana, si—sikumaanisha kufanya hivyo kabisa, naomba unisaidie wala sitafanya hivyo tena”? Yeye ataikataa dhabihu yangu mpaka niende kwanza na kuliweka hilo sawa na mke wangu.

⁶⁷ Basi vipi kama nikimjia na ukosefu uo huo wa heshima, na kusema, “Aisee, msichana wa tangu na tangu wee, rafiki yangu wa tangu na tangu, mama wa watoto wangu wa tangu na tangu, na kipenzi cha enzi na enzi, unajua tumekuwa marafiki

kwa muda mrefu. Aisee, vipi kama nikimkumbatia mwanamke mwingine? Basi wasemaje juu yake, kipenzi, ungenisamehe?”

⁶⁸ Ninawazia jinsi angeniangalia. Angewazia, “Ni nini kilichompata mume wangu?” Unaona? Sasa, kwanza, asingejua kama nilikuwa nikicheza ama kama sikuwa nikicheza.

⁶⁹ Wala huchukui njia hiyo kuungama kwa mwanadamu mwenzako wala kwa Mungu. Unaenda kwa kilindi cha uaminifu, pamoja na toba ya kiungu ya dhambi yako. Kwanza, huna budi kujuta. Sina budi kumwambia, “Kipenzi, njoo hapa, huenda ikamaanisha maisha yetu yaliyosalia ya ndoa. Mwanamke ninayeishi naye, ambaye ni mpenzi wangu, na jinsi nimekupenda miaka hii yote. Lakini sasa unaweza kuniacha, tangu wakati huu na kuendelea, huenda usikae pamoja nami, huenda usinikubali. Nami ninajua jambo hilo. Lakini hata hivyo, kulinyosha, sina budi kuwa sawa.” Inanibidi kumwambia kwa kilindi cha moyo wangu.

⁷⁰ Ndipo inanibidi kumwambia Mungu kwa njia ile ile. Na nimwambie mke wangu pamoja na Mungu, kwa uaminifu, ya kwamba sitafanya jambo hilo tena, kwa neema ya Mungu. Unaona? Kamwe usininii tu kwa kweli... Sasa, huenda nikaweza kumwelezea, naye (mnaona?) hataliona. Labda hotuba yangu kwake ingekuwa—ingemshawishi, bali hotuba yangu haitamshawishi Mungu. Yeye anaangalia moyoni mwangu Naye anajua. Na hata hivyo, miaka mingine michache tu pamoja na mke wangu, Mungu akiruhusu, nasi tutaondolewa humu ulimwenguni. Lakini kwa Mungu, ni Milele, kwa hiyo sina budi kuwa mwaminifu sana kwa Mungu. Na basi kama mimi ni mwaminifu, Yeye atanisikia. Lakini endapo mimi si mwaminifu, hakuna haja kwangu kupoteza wakati wa Mungu akinisikiliza.

⁷¹ Na hapo ndipo imefikia siku hizi, miongoni mwa watu, inaonekana hakuna kilindi cha uaminifu wa—wanachopaswa kuwa nacho.

⁷² Nami ninaamini ya kwamba mwanamume au mwanamke anayekuja kuombewa, wanapaswa kwanza kutubia yote ambayo wamefanya, na kusahihisha kila kitu. Kwa sababu, mnaona, mmeona mara nyingi sana jukwaani, mmeona, angalia hiyo BWANA ASEMA HIVI iko umbali gani. Unaona? Unaona? Hao watu, ono litatokea, bila shaka, kwa imani yao, Mungu aliahidi jambo hilo kwa karama. Bali uponyaji ni kitu tofauti, unaona; Mungu anaitambua basi, unaona.

⁷³ Sasa, tunaona, hiyo ni, watu wanaotubu, hawana budi kuja kwa kilindi cha uaminifu. Ninayo hapa, sina wakati wa kuyasoma, bali yako katika Binghamton, New York, ninadhani. Ama, nimekosea? Naam, Binghamton, ninaamini nimelipata. Mahali ilipo Kampuni ya Viatu ya Endicott. Binghamton, ndio hapo panaitwa Binghamton, Binghamton, hiyo ni kweli, New York. Tulikuwa pale mahali pa viatu pa Endicott-Johnson,

jumba kubwa la mikutano, nasi tulikuwa na mkutano pale. Ndipo asubuhi moja, Billy Paul alikuwa mlango wa pili kutoka kwangu, baridi sana, upepo ukivuma. Basi nilikuwa nimeona, miongoni mwa watu, ukosefu wa uaminifu, ilivyoonekana. Na mimi—mimi nikashangaa ni kwa nini. Huyu hapa mtu mmoja aliyekuwa ameponywa, kusudi, ama mtu mmoja ha—hasa ninayenena habari zake. Mtu huyo alikuwa na mateso makubwa, naye aliponywa usiku huu amesimama pale. Na kabla hatujaondoka, siku tano, mateso yalikuwa yamemrudia tena. Unaona? Kwa sababu, Mbele ya Roho Mtakatifu, aliondolewa hayo. Kama tu ilivyotokea kwa msichana huyu muda mdogo uliopita hapa nje kwenye kitalu, yule kijana mwanamume jana usiku, unaona. Lakini hapana budi kuweko na kilindi cha uaminifu kujua ya kwamba Mungu anayeweza kuuondoa kwako sasa, kwa upako uo huo juu yako, anaweza kuuweka mbali na wewe. Unaona? Na kisha Roho Mtakatifu alinena nami asubuhi moja, mchana, na kusema, “Nenda jukwaani ama mahali fulani, na uwaletе watu hawa hapo na uwafanye watubie kila kitu ambacho wamefanya, kabla hujawaombea.” Unaona? Kilindi cha uaminifu!

⁷⁴ Ulimwengu usipotubu, hauna budi kuangamia. Mnaona? Na toba ndiyo ulimwengu unayohitaji siku hizi, ni toba ya kweli.

⁷⁵ Ni kama vile dawa kwa ugonjwa. Sote tunaweza kusoma kwenye chupa ni dawa ya aina gani na i—itatibu ugonjwa gani. Lakini, mwajua, kusoma maagizo, nitatumia hiyo kama kwa Biblia, shule zetu na seminari zinaweza kulisoma Neno lote. Lakini, mnajua, kusoma tu hayo maagizo na jinsi ya kuinywa, hilo—hilo haliutibu ugonjwa huo. Unaona? Ina—ina dawa, kwa hiyo haina budi kunywewa! Kwa hiyo mtu anaweza kusema, “Mimi ni mwa—mwanatheolojia. Sasa, usinizungumzie, mimi—mimi—mimi . . . kuhusu kadha na kadha, ninayajua Maandiko. Mimi—mimi ninajua ya kwamba Biblia inasema hivi na hivi, *vile*.”

⁷⁶ “Yeye alisikiaye Neno Langu,” Yohana Mtakatifu 5:24, kwa mfano. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Ama, ya King James inasema “dawamu,” ambalo kwa usahihi ni “Milele.” “Yuna Uzima wa Milele kwa kuwa ameamini.” Watu wengi husema wameamini. Sasa, hiyo ni kweli. Ma—Ma—Maandiko ni sahihi. Mimi—mimi ninasoma Ma—Ma—Maagizo, ninasoma Maagizo yalivyo, na Kiuasumu cha dhambi yangu, lakini je! ninaweza kuinywa? Ninaweza kuamini? Huenda nikasema “Ninaamini,” lakini je! ninaamini? Hilo ndilo jambo linalofuata. Kuyasoma tu na kujua maelezo yake, hakuuonyi ugonjwa. Shida ni kwamba (kwetu sisi) hatutakunywa kile Dawa inachosema tunywe. Tuna Dawa, bali hatutainywa. Tunasema tunainywa, kwa sababu tunaweza kuisoma; bali kwa kweli kuinywa, hatuinywi. Unaona, Injili ni vile, dawa, katika kisa hiki. Kama mgonjwa . . .

Nayo dawa hiyo imehakikishwa kumponya mgonjwa huyo, na huyo mgonjwa anasoma yote kuhusu u—uvumbuzi wa dawa hii, nao wanajua kila wakia wa dawa ulio ndani yake, wanajua ji—jina lote la mwanasayansi aliyevumbua dawa hii moja, kama vile dawa ya chanjo ya Salk na kadhalika. Kama sisi—kama tunajua Neno lote juu yake, bali tukatae kuinywa, haitatusaidia. Unaona, Hi—Hiyo haitatusaidia.

⁷⁷ Lakini, na halafu jinsi tunavyosema, “Lakini tuliinywa!” Na kama ukisema uliinywa, naye mgonjwa haonyeshi matokeo, basi hakuinywa. Hivyo tu. Vipi, laiti ile saa ukutani haikuwa inatuingilia hivi, unaona. Ningetaka kukaa hapa na kulishindilia kwelikweli kwa ajili ya watu we—wetu, kwa kuwa Injili imeyathibitisha mambo haya, nao wanadai wanainywa, nao wanaonyesha ya kwamba hawainyi! Mtu anawezaje kuyasoma Maandiko juu ya jambo dogo nililozungumzia, kuhusu wanawake walio na nywele zilizokatwa na kuvaa kaptura, na kadhalika namna hiyo, wanawezaje kujiita Wakristo wakati Dawa Yenyewe inasema kwamba sivyo! Unaona? Vipi? Unasema, “Lakini nilicheza katika Roho, nilinena kwa lugha.” Hilo halimaanishi lolote. Maisha yako mwenyewe yanathibitisha ya kwamba hukuinywa! Unaona? Ulisema u—uliinywa, bali hukuinywa! Kwa kuwa, ungali unaonyesha dalili zote ambazo Dawa hiyo inapaswa kuponya. Nayo hiyo Dawa, katika msimamo wa Injili, ni tiba iliyohakikishwa! Haina budi kutibu. Sasa, unaona, huna budi kuonyesha matokeo.

⁷⁸ Hebu mchukue mtu anayesema ya kwamba wao ni, “Mimi ni. Mimi ni mwaminio. Ninaamini.” Acha Nuru ya Injili iwaguse, ndugu, watainywa sasa hivi! Nao wataonyesha matokeo. Hakika. Hutamwona mtu huyo tena kwenye vyumba vya kamari, hutamwona hapa nje ameshika sigara mkononi mwake, hutamwona akinywa pombe. Loo, la. Hutamwona akifanya ubembe na wanawake wengine. La, la, la. Sijali wataanika miili yao ya kike mbele zake kiasi gani, yeye atakigeuza kichwa chake kuelekea mbinguni na kutazama aliko Kristo. Ni kitu gani? Inaonyesha ya kwamba Dawa ilifanya kazi. Na kama haifanyi kazi, unasema, “Vema, ninajua niliinywa,” vema basi, umefikia wapi leo basi? Unakufa. Unaonyesha! Ninakuangalia wewe kama anayebaini ugonjwa wako, kwa—kwa Biblia, kwamba ungali katika dhambi. Na mshahara wa dhambi ni mauti. Sidhani inapaswa kuelezewa kinaganaga zaidi. Unaona, matendo yako mwenyewe yanathibitisha, matendo yako mwenyewe yanathibitisha ya kwamba hukuinywa. *Ulifiki* uliinywa. Amina. Hu—huenda ulikuwa mwaminifu sana katika kufanya hivyo, bali hukuinywa! Kwa kuwa, kama ungaliinywa, Mungu aliahidi ya kwamba ingekuwa na matokeo kwako. Nayo ile dhambi ya kale ingalipo pale, ile tabia ya kale ya Adamu ingali inadumu pale, kule kutokuamini kwa kale. Hata hivyo unajaribu kujifanya mwenyewe, mbele ya wenzako, kusema,

“Vema, mimi ni mwaminio. Loo, utukufu kwa Mungu! Naam, mimi ni mwaminio.” Lakini, unaona, haikukusaidia hata.

⁷⁹ Labda huyo mgonjwa mwenyewe kamwe hakuwa amekusudiwa tangu awali ku—kuinywa hiyo Dawa. Kama ndivyo ilivyokuwa, kamwe isingesaidia. Hiyo ni kweli. Unaona?

⁸⁰ Lakini mwangalie yule mwanamke mzinzi wakati ile Nuru ilipomgusa, kulikuwa na kitu kilichokuwa pale kushughulikia hali yake. Unaona? Kama tukiamini na tutubu kwa uaminifu, Dawa hii ya njia ya Mungu hufanya kazi. Mungu ameandaa njia kwa ajili ya mambo haya.

⁸¹ Sasa, unaona, mtu ataenda, aseme, “Vema, nilijiunga na kanisa. Hilo latosha kwangu.” Hiyo si njia iliyoandaliwa na Mungu.

⁸² Njia ya Mungu iliyoandaliwa ni toba, maungamo, na kuonyesha matokeo, kuzaa matunda yapasayo toba, kuonyesha uaminifu. Kama ninyi watu mtafanya hivyo asubuhi ya leo, mtakaombewa! Na ninyi watu mnaoisikia kanda hii, kote ulimwenguni, na baada ya kanda hii kuchezwa na mhudumu ama mtu anayeicheza katika makundi ya kusanyiko huko misituni ama popote mlipo, mnaoicheza, kwanza mtafanya toba yenu dhahiri, kisha mje bila chochote moyoni mwenu, ila imani, na kuombewa, hapo ndipo Dawa itakapofanya kazi.

⁸³ Yesu alisema, “Tubuni, kila mmoja wenu!” Ninamaanisha Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Unapotubu kwelikweli na kumwamini Bwana, na ukabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, unamfanya Mungu mwongo kama humpokei Roho Mtakatifu. Kama... Yesu alisema hivi, agizo la mwisho kwa kanisa Lake, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Nawe ukiona ishara hizo zikimfuata mwaminio, nawe unakuja na huyo mwaminio anakuwekea mikono, na jambo fulani halitukii, basi imani yako ina kasoro fulani. Unaona? “Mwaminio!” Mungu aliahidi njia iliyoandaliwa.

⁸⁴ Tunajaribu kupata faraja kwa kusema, “Si lazima nisikilize.” La, hiyo ni kweli, si lazima usikilize.

⁸⁵ Lakini kama umechaguliwa tangu zamani kwa Uzima wa Milele, utalisikiliza na utalifurahia. Ni Faraja yako. Ndicho kitu ambacho umetamani maishani mwako mwote. Ni—ni ile Lulu, kwamba, uko—uko tayari kuachana na kila kitu. Unaona? Unalitaka kwa sababu unajua kwamba ni ulinzi wenye upendo wa Mungu kwa ajili yako. Ndicho kitu cha kulitatua suala la dhambi, kutatua kutokuamini, kutatua kila kitu, kwako, kama unakitaka. Ni mtu aliye mgonjwa kwelikweli na ajuaye kwamba ni mgonjwa, ndiye atafutaye daktari. Unaona? Si mtu asiye mgonjwa, hamhitaji, Yesu alisema. Lakini ni wale walio

wagonjwa. Kama unaweza kuitambua hali yako, basi huna budi kufanya kama alivyosema ufanye. Ndipo haina budi kutukia, la sivyo Mungu alisema jambo ambalo lilikuwa ni kosa. Unaona?

⁸⁶ Watu wengi sana wakati mwingine, ibada za uponyaji, huanzii kwenye msingi wake. Mtu inakupasa kuyasafisha maisha, huna budi kuwa katika hali nzuri, kweli huna budi kusema, “Naam, ninaliamini,” na hilo linapaswa kutoka moyoni mwako. Halafu wewe, hakuna mtu anayepaswa kukubembebeza-bembebeza, akisema, “Sasa, loo, ndugu mpenzi, dada mpenzi, unapaswa kufanya *hivi*, unapaswa kufanya *vile*.” Wewe ni mwaminio, hakuna kitu kinachoweza kuliondoa kwako. Sijali yale mtu mwingine yeyote angesema, yale maliwazo yoyote, yale mfariji yeyote, yale daktari yeyote, yale hospitali yoyote, yale ubaini wowote ungesema, ungali huamini hayo. Unajua tu Hilo! Hakuna haja ya kusema jambo lingine lolote kulihusu, unalijua! Sasa, hilo ndilo jambo halisi.

⁸⁷ Tuna kuiga kwingi sana katika mambo yote. Haina budi kuwa hivyo. Usijisikie vibaya kuhusu Hilo. Halina budi kuwapo hapo. Daima limekuwako na litakuwako. Lakini ninakwambia asubuhi ya leo yaliyo Kweli na mambo yaliyo hakika. Tuko katika wakati wa mwisho. Hatuna budi kuweka jambo hili moja kwa moja kwenye Kweli, unaona, na wapate kujua kilicho Kweli.

⁸⁸ Sasa tunaona ya kwamba watu hawataichukua njia ya Mungu kuhusu jambo hilo. Wanataka, wao...Mungu ana njia iliyoandaliwa kwa ajili ya faraja yako. Mungu ana njia iliyoandaliwa kwa ajili ya mambo haya yote. Lakini watu hawaitaki, watu wanafuata njia zingine. Na kila wakati wanapolifanya kwa njia nyingine mbali na njia ya Mungu, wanaleta hasira ya Mungu juu yao kila wanapofanya hivyo. Vema.

⁸⁹ Na mambo haya yote ambayo nimenena habari zake, yanatuleta kwenye jambo hili, ulimwengu, wote hawa wakiufuatilia ufanisi mwingine wa sayansi, wakiufuatilia ufanisi wa kanisa, kufuatilia mambo mbalimbali kumetufikisha kwenye mwisho wa ulimwengu. Tuko mwisho. Hakuna tumaini hata moja lililosalia. Hatuna tumaini la kupona. Hatuna hata nafasi moja ya kupona. Sasa hebu niyaelezee haya kwa dakika chache tu, na kuwathibitishia.

⁹⁰ Na kila mmoja wenu, hebu chukua, kama huninii, unapaswa kuchukua jarida la matibabu, unapaswa kuchukua Reader's Digest, na kadhalika, ambamo mnasoma mafanikio haya. Sasa kufanya...

⁹¹ Mhudumu fulani hapa anautuma Ujumbe huu kote ulimwenguni. Kutoa tamshi kama hilo, kwamba hatuna matumaini, kwamba hatukomboleki, kwamba tumepita mstari kati ya ukombozi na hukumu, sasa sina budi kulipa kusanyiko hili sababu chache za kuwekea msingi tamshi hili. Lazima

kuwepo na sababu ambayo mtu, kama yuko na akili timamu jinsi ninavyofikiri ninazo, angetoa tamshi kama hilo, kuliambia taifa lake, kuliambia kusanyiko lake, kuwaambia watu ambapo utaenea kote ulimwenguni katika mataifa thelathini au arobaini mbalimbali, labda, kote ulimwenguni, na watu na lugha, ya kwamba “tuko katika wakati wa mwisho,” inatupasa kutoa tamshi ama—ama—ama kuelezea kidogo mpaka tutakapofikia somo letu halisi la asubuhi hii.

⁹² Angalieni, sasa hebu tuangalie yale sayansi na elimu zimetuletea, na hicho ndicho kitu hasa ambacho mwanadamu alikikubali badala ya Neno la Mungu, kibali cha kisayansi. Na sayansi daima imelazimika kughairi yale waliyosema. Nilikuwa nikisoma hapa wakati fulani uliopita ambapo mwanasayansi Mfaransa alisema, yapata miaka mia mbili iliyopita, ama mia tatu, “Kuufingirisha mpira kuizunguka dunia,” basi akasema, “kama mpira huu, kwenye mwendo huu... Kama ulimwengu ungepata kuvumbua namna fulani ya kitu ambacho kingewafanya wasafiri kwa angalau maili thelathini kwa saa, kitu kama hicho, kuizunguka dunia,” ambalo alilithibitisha kisayansi, “kwamba hicho kwa uzito wake kingeinuliwa na nguvu za uvutano kitoke ardhini.” Unaona? Sasa, mnafikiri sayansi kamwe ingemrejea jamaa huyo? La hasha. Kwao, hayo yemepita zamani.

⁹³ Sasa, hebu na tufikirie tu sasa, sote tunataka kusema, “Ninataka kulithibitisha kisayansi.” Hivyo ndivyo watu wengi wa dini za kimadhehebu husema siku hizi. Wanataka thibitisho la kisayansi. Vema, ningeweza kugeuka moja kwa moja na kusema, “Nithibitishie kisayansi, Mungu katika kusanyiko lenu. Nithibitishieni chochote, kisayansi, ambacho ni halisi. Thibitisheni...”

⁹⁴ Ni kitu gani kilicho halisi? Uhai. Ninakutaka unipatie robo ya thamani yake, ama—ama acha niuze kila kitu nilicho nacho, ili nipate sehemu hiyo ya uhai. Na je! uhai ni halisi? Kama si halisi, sisi sote tuko hapa kwa sababu gani?

⁹⁵ Uhai, imani, upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, unyenyekevu, saburi, sayansi haiwezi kuyagusa. Na hicho ndicho kitu pekee halisi, cha kudumu kilichopo. Silaha yote ya Mkristo ni kuangalia yasiyoonekana. Lakini hisi hazitangazi mambo hayo, bali yapo. Hiyo ndiyo sababu inahitaji imani kuamini jambo hilo, na linasababisha ndani yako kile imani imetangaza kuwa kiko huko nje. Inakuletea, uponyaji wa Kiungu na kadhalika. Hawawezi kuthibitisha ni kitu gani kinachoponya Kiungu, bali wanajua kuna uponyaji wa Kiungu. Mimi... Hawawezi kuthibitisha ni kitu gani kinachookoa kutoka dhambini, bali wanajua watu wanaokoka kutoka dhambini. Kwa hiyo haliwezi kuthibitishwa kisayansi, bali ni la kisayansi katika njia ya Mungu ya kuiangalia.

⁹⁶ Sasa, sayansi imetuletea nini? Sasa, huenda mkashtuka sana kwa dakika moja. Sayansi imetuletea maradhi, mauti, na magonjwa. Sasa, mmefundishwa tu upande mmoja wa picha. Lakini kuna pande mbili zake. Mnasema, “Sayansi imevumbua *hiki, kile na kinginecho*. Vema, tutakupa majaliwa hayo. Lakini hebu na tuangalie huo upande mwingine. Sayansi imetuletea maradhi. Sayansi imetuletea magonjwa, mauti.

⁹⁷ Angalia! Uzalishaji wa kisayansi umeleta mauti kwa kizazi hiki, wa chakula na kadhalika. Umewafanya watu wanyonge sana na ninii sana, hata wa—wanaume na wanawake wamefanywa kwa lundo la uchafu, wala hakuna—hakuna—hakuna umbile kwake. Imekuwa ni kundi tu la viwavi wanyonge. Hawawezi kuishi bila ya kiyoyozi, wangeangamia. Hawawezi kucheza mchezo wa besiboli, kama mmoja wao akigongwa mahali fulani, ingemuua, katika lingo za masumbwi na kadhalika. Na ni wanyonge sana hata wanaume na wanawake, vema, inawapotosha.

⁹⁸ Nao wanaingiza kwa kupiga sindano hizi mbegu za mchanganyiko katika ng’ombe ambazo zimewarudia wanadamu sasa, kulingana na sayansi yenyewe, nazo zinawapotosha. Kwa sababu, wakati ng’o—ng’ombe ni chotara, ama chakula chochote ni chotara, chakula hicho kinafanya seli ya damu, na seli ya damu ndiyo uhai wako. Mnaona vile imefanya? Halafu basi, katika nyama, wanapiga sindano na kuingiza vitu hivi hapa katika nyama, na sasa imethibitika ya kwamba vitu hivi wanavyoingiza vinaiathiri jamii ya binadamu. Vitu vya kisayansi!

⁹⁹ Wananyunyizia mashamba hii DDT, niliona hivi majuzi, na sasa tuna watu mia nane wagonjwa katika jamii hii kutokana na kula mayai. Je! mnakumbuka miaka kadhaa iliyopita mara ya kwanza nilipokuwa, wakati tulipokuwa na jengo dogo hapa, nami nilikuwa nikitabiri, na kusema, “Itakuwa katika siku za mwisho, msiishi bondeni wala msile mayai.” Nimeuandika katika kitabu changu. Nilifikiri kulikuwako na jambo fulani kuhusu jambo hilo, nami nikaenda na kuliangalia. “Msile mayai.” Hayo yalikuwa ni huko nyuma kabisa mwaka wa 1933. Mayai yana kitu fulani ndani yao sasa, nami naona ambapo sayansi inasema ya kwamba mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka hamsini hapaswi kula yai kamwe, kwa sababu ndicho kitu kigumu sana kwenye moyo kinachoweza kuliwa. Magonjwa!

¹⁰⁰ Maziwa, ilikuwa kwamba mlo wetu kamili sana ulikuwa ni maziwa. Madaktari watakwambia, “Achana nayo.” Yanasababisha mapindi na kadhalika. Ni mwanadamu yule yule aliyekuwa akiyanywa na kuishi kwa miaka mingi wala kamwe hakujua mapindi, bali kule kuzalisha na kadhalika kumevunjilia mbali maumbile ya mwanadamu mpaka yeye si kitu ila lundo la uchafu, mpira—mpira wa maradhi. Ni kitu gani kimesababisha jambo hilo? Sayansi!

¹⁰¹ Angalieni! Imesababisha jeni kati ya mwa—mwanamume na mwanamke kudhoofika, unyonge wa mwili wa mwanadamu, kupitia jeni, na ongezeko la watoto wenye kifafa ni kwenye asilimia thelathini. Kuzaliwa na vichwa bapa kunaongezeka sana. Na unyonge huu wa kuchanganya mbegu wa vyakula tunavyokula kwa ajili ya uhai, kunaudhoofisha mwili, jambo ambalo linasababisha kansa, magonjwa ya akili, na kila namna ya magonjwa yanaingia kwenye mwili wa binadamu kwa sababu ya unyonge wake. Wa kisayansi, wanajiangamiza, wakiuacha mpango wa Mungu.

Yeye alisema, “Na kila mbegu ize kwa jinsi yake.” Um-hum.

¹⁰² Mnaona mahali tulipo? Ningeweza kuendelea mbele zaidi na zaidi; wakati wetu unaisha. Lakini, angalieni, ni kitu gani kinachosababisha jambo hilo? Sayansi imeleta mauti, maradhi, na maangamizi.

¹⁰³ Nami niliona hivi majuzi, nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu msiri, Daktari Vayle anayeketi hapa, kwamba kuna makala ya kwamba watu wanauawa na penisilini. Kwa kweli si penisilini, ni uchafu wanaoruhusu kuingia ndani yake wakati wanapoitengeneza penisilini. Ni mbinu za tamaa, kupata fedha. Madaktari wakiitoa ambao hata hawajui fomula ya asprini, na huku baba yao aliwatuma huko kupata u—utaalamu wa kitu fulani, wala hata hawajui jinsi ya kutibu ugonjwa wa kuumwa tumbo kwa mtoto. Lakini tuna kitu gani? Tamaa, mvuto fulani, ama kitu kidogo. Ni vigumu kumpata tena daktari wa mtindo wa kale wa kijijini ambaye alikuwa akishuka kuja na kuzungumza nawe na kukufariji na kufanya kila kitu. Wanamwacha Mungu nje kabisa, kwa sababu walifuata njia yao wenyewe. Kusudi wamwondoshe Mungu jukwaani, walimwelezea vibaya kabisa. Haya basi.

¹⁰⁴ Hivyo ndivyo tumefanya kwa kuchanganya mbegu. Mnaona, mwili... Kile kinachofanya mmea wenye afya, ni vigumu kwa mdudu kuuvamia. Ni hii mimea ya tuta, mimea hii chotara inayokubidi kuinyunyizia sikuzote. Na wengi wenu mmekisoma kitabu changu cha *Dini Chotara*, mnaendelea kuinyunyizia na kuibembeleza na—na kadhalika. Angalia, bali mmea halisi na wa kweli sio lazima unyunyiziwe, huo ni wa asili.

¹⁰⁵ Ni kitu gani kinachoufanya ugonjwa uingie katika mwili wa mwanadamu? Ni mwili... Kama ninavyoambiwa na rafiki yangu daktari wa thamani, ambaye nisingetaka kutaja jina lake sasa hivi, bali yeye ni ndugu mzuri sana, akinisoma mimi hivi majuzi kutoka kwenye jarida la matibabu, kitabu fulani ofisini mwake ambako anaweka vitabu hivi vyote vizuri na makala ya karibuni sana ya matibabu. Ni unyonge. Unaona mtu yeyote ambaye ni ninii sana... Unasema mwili wako umedhoofika, unashikwa na mafua upesi sana. Ni kitu gani? Udhaifu wa mwili wako ndio unaosababisha kamasi kutoka kwenye tezi zako. Na, katika hilo, seli zazi ya homa inakwingia nawe unapata mafua.

Lakini kama mwili huo ulikuwa na nguvu, ungeitupilia mbali hiyo seli zazi ya homa, isingeweza kuugusa.

¹⁰⁶ Kwa hiyo, unaona, wakati Mungu alipomuumba mtu kwa mara ya kwanza, alikuwa na kinga ya ugonjwa wowote. Unaona? Lakini kutokuamini na sayansi, sayansi na elimu zilikuwa ndicho kitu cha kwanza kilichomwondoa mwanadamu kwa Mungu, na zingali zikimwondoa.

¹⁰⁷ Angalia tu kile sigara na unywaji wa pombe, na hawa wavua nguo na kadhalika, vimefanya katika kuzorota kwa kizazi hiki. Nadhani daima mnashangaa... Nitatoa tamshi hapa. Sikuwa nilitoa, bali ninaamini nitalitoa.

¹⁰⁸ Unaona, wao wanashangaa wakati mwingine, daima wananiambia, “Ndugu Branham, ni—ni nini kinachokufanya sikuzote kukemea vitu hivyo namna hiyo? Huyasikii... Tuseme unaenda kwenye kanisa la mtu fulani, mbona, ninaweza kuwachukua wanawake wangu nao hata hawawezi kuketi kwa faraja mahali unapohubiri. Daima unawakemea sana, vema, kuhusu nywele zao fupi, na kuhusu kuvaa nguo zinazompasa mwanamume, na mambo haya yote namna hiyo. Aisee, kwa nini unafanya hivyo?” Sasa mimi—mimi—mimi ni... .

¹⁰⁹ Huenda huu ukawa ndio Ujumbe wangu wa mwisho mpaka msimu ujao wa kiangazi, mwajua, bali ninataka kuwaambia. Hili hapa. Ni Roho wa utambuzi kwa ajili ya siku hizi za mwisho, ambayo inajua ya kwamba hilo ni jambo lililolaaniwa mbele za Mungu. Wakati mwingine ninashangaa tu kama mhudumu ana utambuzi wowote wa siku za mwisho? Mungu yeye yule anayesema jukwaani hapa hali zako na yale umefanya, na—na kile utakachokuwa, na—na shida ulizo nazo, Roho yuyo huyo aliye ndani yako anaangalia nje na anaweza kuzitambua ishara za wakati, wala hawezi kusita kuyakemea. Ni Roho wa utambuzi, maana Roho Mtakatifu Mwenyewe anasema kitu hicho ni dhambi, na yeyote anayekishiriki ataangamia. Basi ninawezaje kuhesabiwa haki mbele za Mungu, na huku ninawaona dada na ndugu zangu katika hali ya namna hiyo, kama silikemei? Ingawa wananikasirikia, ningali sina budi kulikemea. Ni utambuzi. Wakati mwingine wanatofautiana kwenye Neno na kadhalika, na ni ukosefu wa utambuzi. Njoo ukalikabili kwa Neno. Unaona? Unaona, sisi tu—tunajua hiyo ni kweli. Vema, ni, imejulikana ni kweli. Ni utambuzi wa siku za mwisho.

¹¹⁰ Sasa tunaona kuhusu sayansi, si—sitaki kwenda mbali zaidi juu ya hilo, wakati wangu unaenda mbio sana. Sasa hebu tuitupie jicho elimu mara ya pili tuone kile imefanya. Unaona? Sasa tuna makanisa mawili kwa jumla.

¹¹¹ Sasa, tunatambua ya kwamba ilikuwa ni hiyo, kwamba ilikuwa ni hoja, hoja ya kawaida iliyoanzisha mpira wa dhambi kuvingirika hapo mwanzo. Ilikuwa ni hoja ya nini? Hoja

dhidi ya Neno la Mungu. Wakati Mungu alipowaambia Adamu na Hawa, “Siku mtakayokula kwake, siku hiyo mtakufa,” Hilo lilitosha, hakuna lingine. Naye aliwakinga na adui, nyuma ya Neno Lake. Bali wakati Hawa, akisikiliza hoja za Shetani, unaona, utamaduni, ufahamu, elimu, maendeleo, unaona, mwanamke alitoka akaenda pale nyuma na kusikiliza hoja za Shetani, na kufanya jambo ambalo Mungu alisema “msilifanye.” Na kama hoja moja, kusikiliza hoja moja dhidi ya Neno kulisababisha mchafuko huu wote, hoja moja dhidi ya Neno tena haitakurudisha mahali pale pale, maana ingekuwa ni ujinga jinsi gani kwa Mungu kumrudisha mwanadamu juu ya msingi ule ule aliomtoa kwao. Unaona? Unaona? Huna budi kuja kwenye Damu iliyomwagika ya Kristo. Dhehebu lako halitafaa kitu, na hoja zako hazitafaa kitu. Ni ile Damu na kuzaliwa, nayo inazaa ndani yako kiumbe kipya, Kristo, nawe unaishi kwa mfano wa Kristo, kwa sababu Sumu unayokunywa inaonyesha inaua dhambi ya kutokuamini, dhidi ya chochote ila Neno la Mungu.

¹¹² Elimu inatupa . . . Tuna makanisa mawili mbele zetu asubuhi ya leo. Moja la hayo ni Kanisa la pentekoste lililowekwa katika utaratibu na Roho Mtakatifu pale Pentekoste; la pili ni kanisa la Katoliki la Kirumi ambalo liliunda dhehebu huko Nikea, Rumi. Moja la hayo ni kuzaliwa kwa roho; hilo lingine ni ufuasi wa kielimu. Kutokana na kanisa hilo wanakuja waprotestanti wote, madhehebu yote yanatokea. Hilo lilikuwa ndilo dhehebu la kwanza. Madhehebu yote yanatokana na hilo na yanahusiana na hilo, Ufunuo 17 inasema hivyo, “Yeye alikuwa ni kahaba na alikuwa ndiye mama wa makahaba.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hakuna . . . Nyungu haiwezi kuiita birika ati ina grisi, unaona, kwa sababu ni—ni kweli, ni moja tu. Limeunda dhehebu, limekwisha, liko Roma. Sijali ni kitu gani, limekwisha! Biblia, ndio kwanza tuzipitie zile nyakati za kanisa, kuthibitisha jambo hilo. Moja lina msingi wake kwenye utambuzi wa kiroho; hilo lingine limewekwa msingi juu ya elimu na dhana za kiakili.

¹¹³ Sasa, hilo linaturudisha moja kwa moja katika Bustani ya Edeni tena, moja kwa moja mahali pale pale. Yule mwanamke (kanisa) ndiye aliyesikiliza, si Adamu, mwanamke! Sasa wanataka kuwa kanisa mama, haya endeleeni! Ni kweli kabisa. Hakuna kitu kilicho nje ya wakati. Wao wenyewe wanakiri, mnaona. Mnaona, kurudi moja kwa moja kwenye kitu kile kile, kwenye kutokuamini Neno la Mungu! Huko Nikea, Rumi, wakati suala lilipoibuka kuhusu ubatizo wa maji, kuhusu mambo mengine kama hayo, na kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, ma—maaskofu kwa jumla waliliunda dhehebu lililoitwa kanisa Katoliki la Kirumi, ambalo lilikuwa Rumi “ya kifalme,” ndiyo lilivyoitwa. Ndiyo kwanza tumalizie kuichukua historia jana, na kuisikiliza, tukiichunguza tena. Na ilikuwa tu iwe ni ya Rumi pekee, katika Rumi kulikuwako na kanisa la

kifalme. Hayo mengine yalikuwa tu makanisa madogo mashirika kwake, yaliitwa tu Katoliki.

¹¹⁴ Kanisa letu pia ni katoliki, Kanisa la ulimwenguni kote, ambalo ni i—imani ya kote ulimwenguni ya waaminio wote. Moja la hayo limezaliwa kwa Roho wa Mungu na lina Roho Mtakatifu ndani Yake, na linathibitisha jambo hilo kwa maisha Yake, Fundisho, na matendo, ya kwamba Roho Mtakatifu yuko mle ndani, kwa sababu Ndiye Mfariji ambaye Kristo—Kristo aliahidi, akitenda kazi kanisani Mwake, akifanya jambo lile lile alilofanya hapo mwanzo. Hivyo ndivyo Sumu ya wokovu wa Kristo ilivyofanya kazi hapo mwanzo, hivyo ndivyo inavyofanya kazi siku hizi, inazaa kitu kile kile.

¹¹⁵ Hilo lingine ni dhana ya kielimu ya dhehebu lililofanyizwa na kundi la watu, lililo na “mfano wa utauwa,” kama nabii alivyotwambia, “na lilikana Kweli hii ya Nguvu.” Sasa, hilo ni dhahiri tu kama ninavyojua kulifanya.

¹¹⁶ Sasa, hayo hapo hayo makanisa mawili. Moja la hayo lilizaliwa huko Nikea; na hilo lingine lilizaliwa Pentekoste. Na—na moja daima limelipinga hilo lingine. Tumepitia kwenye nyakati za kanisa kuthibitisha jambo hilo, moja linalipinga hilo lingine. Moja la hayo ni kanisa zuri, lililotukuka, la kielimu lenye wanazuoni hodari na kadhalika; hilo lingine linahesabiwa kama “kundi la watakatifu wanaojifingirisha.” Lilikuwa hapo mwanzo, “wavuvi walevi wasio na elimu,” na ni jambo lile lile siku hizi, lingali linahesabiwa katika kundi lile lile. Moja la hayo ni la kisayansi; hilo lingine ni la kiroho. Moja ni mpangililo wa kisayansi; hilo lingine ni utambuzi wa kiroho wa Neno. Moja limepangwa kisayansi, yale makundi ya mwanadamu yanayosema, askofu wa kielimu. Hilo lingine limezaliwa kabisa na Roho wa Mungu, nalo linaishi kwa Roho wa Mungu, na linatenda na kutimiza Maneno ambayo Mungu aliahidi. Inaonyesha unakunywa sumu gani. Je! una sumu ya kielimu? Je! una Sumu ya Roho Mtakatifu? Unaona? Vema.

¹¹⁷ Loo, huo ujanja wa Shetani! Jinsi anavyoweza kuichora picha hiyo, kielimu anaweza kumfanya mtu asiyezaliwa kwa Roho wa Mungu kuzunguka na kuzunguka! Wala hakuna njia, kiakili, ya kuwashinda nayo. Hakuna njia.

¹¹⁸ Ni utambuzi kwa imani, mnaona, utambuzi. Tunaona kile Neno linachosema, tunakiamini.

¹¹⁹ “Halafu, Ndugu Branham, wao wanasema wana utambuzi.” Basi acha Roho Mtakatifu atoe hasa kile alichohidi kutoa, ndipo tutaliadini. Unaona? Huo hapo ushuhuda wa jambo hilo.

¹²⁰ Hiyo Sumu ilitendaje kazi wakati ilipomgusa mtu? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” Yeye alisema. Kama Sumu iligusa hilo, basi hilo ni sawa. Unaona? Kwa hiyo wanatuleta . . .

¹²¹ Hili linatuleta sasa, katika kufunga, kwa dakika chache zifuatazo, kwa hiyo hii inatuleta kutoka kwa Habili na Kaini,

hadi kwenye ile hukumu ya wakati wa Nuhu, kutoka kule kuja kwenyewe kwa siku za Nuhu. Sasa, kabla hatujaufanya mstari wa maombi, sikilizeni kwa makini ninapopitia kwenye Maandiko fulani hapa kwenye—kwenye fungu dogo.

¹²² Tunaona ya kwamba baada ya ulimwengu kuchukua wazo lake la kielimu la Neno, hao watu wakawa watu mashuhuri, watu wenye sifa. Biblia inasema hivyo, Mwanzo 6:4. Watu wenye sifa wakiwaandama wanawake warembo sana na kadhalika, kama ilivyokuwa kote ulimwenguni. Ndio kwanza tuupitie kwenye *Vimulimuli Vyekundu*, tulizungumza hivi majuzi usiku jinsi wanawake walivyokuwa wawe ni warembo zaidi katika siku za mwisho, jinsi wanaume, watu wenye sifa, kama vile ile kashifa Uingereza na Marekani. Na ingali itagunduliwa moja ya siku hizi. Mnaona, hamjui yale hawa malaya wote watongozwao kwa simu na kadhalika wanahusu. Mnaona? Je! mnajua kuna wahudumu wasichana wa baa watatu-kwa-mmoja kuliko wasichana wa sekondari ya juu na wa chuoni? Wahudumu wasichana wa baa watatu-kwa-mmoja kuliko msichana wa sekondari ya juu na wa chuoni. Je! mnajua, asilimia fulani, siwezi kuikumbuka sasa maana haipo mbele yangu, kamwe sikuandika, lakini karibu theluthi moja ya watoto wa sekondari ya juu kote nchini ama imethibitishwa kwamba ni malaya au iliwabidi kwenda nyumbani wakajifungue? Je! mnajua ya kwamba kunywa penisilini kukomesha magonjwa ya zinaa kumesababisha tu upotovu miongoni mwa watu, ambapo, kitu hicho hakijafa? Lakini hata hivyo, mnaona, Mungu alisema itakipatiliza hadi kizazi cha nne. Inasababisha kuzaliwa punguani mwenye kichwa bapa na chochote kile, nao watoto wananinii... Loo, jinsi ambavyo dhambi, jinsi ilivyo janja! Jinsi ambavyo hao watu, hao wahudumu watasimama wala wasihubiri dhidi ya hao wavua nguo mtaani, na kuwaacha waimbe kwenye kwaya, na kila kitu jinsi hiyo, na kuona hicho ndicho kitu kile hasa kilichoitupa nchi yetu kuzimu, kikaitupa jamii yetu kuzimu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo sasa tunaona ya kwamba baada ya Mungu kuchoshwa nayo, kama ninayoamini yamemchosha siku hizi. . .

¹²³ Sasa ninalifikia somo langu. Nina njia ya kiajabu ya kuleta... Ninapenda kuyakusanya mambo mengi halafu ninalifikia somo langu. Sasa, tunaona ya kwamba katika siku za Nuhu, wakati Mungu alipokuwa akitaka kuuhukumu ulimwengu, wakati ulipofikia tu kama ulivyo sasa, maana Yesu alisema ulikuwa hivyo, je! Yeye alijali? Alijali? Yeye, hakika alijali. Alijali nini? Sasa, Yeye akiisha kujua ya kwamba hukumu ilikuwa inakuja, naye alikuwa ametangaza hukumu, Yeye aliwajali wale waliojali. Na hivyo ndivyo vile vile ilivyo siku hizi. Aliwajali wale waliokuwa tayari kujali. Nasi tunaona ya kwamba aliwatumia nabii kuwaongoza, kuwaongoza wateule Wake kwenye njia iliyoandaliwa ya wao kuepukia. Ni yeye yule

jana, leo, na hata milele. Mnaona? Tunaona ya kwamba Mungu aliwajali watu Wake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

124 Tuko mwisho, nasi tunaona tuko mwisho! Hakuna njia ya kujengea juu ya upotovu huo. Tunawezaje kujenga jiji juu ya magofu yaliyounguzwa ya Sodoma na Gomora? Tunawezaje kufanya jambo hilo? Kuna finiksi moja tu iliyobaki, na hiyo ni kule kuja kwa Bwana Yesu; loo, jamani, kutakaswa kupitia kwenye ule wakati wa Dhiki, kurejesha kurudishwa kwa ulimwengu, kwa ajili ya watu walio na haki mbele za Mungu na wanaoishi kwa Neno Lake.

125 Angalia, Yeye aliwajali wale waliojali kuponyoka katika siku za Nuhu, naye akawatumia nabii. Naye huyu nabii akawaongoza kwenye njia iliyoandaliwa na Mungu. Sasa, hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kufanya mambo. Unaona? Mungu alinena na Nuhu, ambaye alikuwa ni Neno (wakati huo halikuwa ni Neno lililoandikwa), na akamwambia Nuhu aandae safina kwa ajili ya kuwaokoa watu, na kuwaonya watu wote ya kwamba Yeye alikuwa na “njia moja ya wokovu.” Naye mtu huyu alikuwa ni nabii aliyethibitishwa aliyewathibitishia njia ya kuponyoka. Angalia, watu wanyenyekevu na waaminifu walimsikia mtu huyu na kumwamini, nao wakapona. Walipona na kitu gani? Mauti ya ulimwengu wa dhambi ambao ulikuwa ukiangamizwa katika siku hiyo, waliepuka njia ya mauti iliyokuwa imewekwa mbele ya ulimwengu mzima. Mungu alijali sana! (Ee Mungu, jalia hili lingie ndani kwenye kilindi sasa, kabla ya mstari wa maombi.) Mungu alijali!

126 Yeye anauangalia ulimwengu sasa siku hizi, Naye ameita na ameita, nao wakadharau na kukataa. Palikuwapo na nafasi ya kutubu hapo mwanzo. Wakati Mungu alipomwambia Isaya aende na aweke...kumwambia Hezekia atakufa, Hezekia alitubu na kulikuwako na rehema. Wakati Mungu alipomwambia Yona aende Ninawi na kupaza sauti, maana katika siku arobaini Yeye angeangamiza mji huo, wao walilia sana wapate rehema na kulikuwako na toba. Bali wanapoikataa, hakuna kilichosalia ila hukumu! Nalo taifa limemkataa Kristo. Wameshindwa kuuitikia ule mwito, kwa hiyo hakuna kilichosalia ila hukumu inatukabili.

127 Sasa, je! Mungu anajali kuhusu wale ambao wametubu? Je! amewaandalia njia? Sasa tutaenda kuona kile alichofanya katika nyakati zilizopita.

128 Wakati wa Nuhu, Yeye alijali! Alimtuma nabii, na Yeye—Yeye akaileta njia na kuwaonyesha njia, naye akawaonyesha njia ya kuepukia nao wakaepuka ile hukumu. Pia aliwajali. Tunaona ya kwamba Yeye huwaleta mahali ambapo Yeye, katika siku za mwisho, ambapo (pote) kabla ya ile hukumu iliyo kuu haijakuja, Yeye aliwajali sana mpaka akaandaa njia ambayo wangeingia na wangekuwa huru na hukumu zote zilizokuwa zikija.

¹²⁹ Sasa, Yeye alifanya hivyo kwa Wa—Wateule. Sasa, tunajua jambo hilo. Alifanya hivyo kwa Wateule, kwa Wateule peke yao, sasa! Ndio waliokuwa wameikubali seli zazi hii ya Uhai. Ndio waliokuwa wamekusudiwa tangu awali kuliona. Hao ndio waliokusudiwa. Sisi sote, kama tukiamini Biblia, hatuna budi kuamini katika kuchaguliwa tangu zamani. Unaona? Hiyo ni kweli. Si kwamba Mungu angependa yeyote ateseke, bali Yeye alijua ni nani angeipokea na ni nani asingeipokea.

¹³⁰ Pia aliwajali wateule Wake katika siku za maangamizi ya Misri. Walikuwa kule chini Misri nao wakawa watumwa. Siku za Musa, Yeye aliwajali watu. Aliwatumia nini? Nabii, tena. Hiyo ni kweli? Naye aliwatenganisha watu Wake na ulimwengu usioamini, kutokana na hukumu ijayo ya siku hiyo. Je! alifanya hivyo? Alijali wakati Misri walipokuwa wamelundika dhambi zao juu sana mpaka ikambidi Mungu kutuma hukumu, kwa maana tayari alikuwa amemwambia Ibrahimu, “Nami nitaliadhibu taifa hilo.” Kwa hiyo badala ya kuimwaga ghadhabu yake juu ya hao wote, Yeye aliwatumia faraja Yake. Aliwatumia Mfariji Wake. Aliwatumia Neno Lake. Naye daima hulituma Neno Lake kwa nabii Wake, kama alivyofanya katika wakati wa Nuhu. Alifanya jambo lile lile katika siku za Nuhu. Katika siku za Eli...za Musa, tunaona Yeye alifanya jambo lile lile. Aliwatumia nabii Wake, nao wakajitenga na kutokuamini. Sasa, watu wa jinsi hiyo ndio waliotoka. Hao ndio walioliamini. Walimwamini Musa, kwamba yeye alikuwa ni...Machoni pa Farao, alikuwa ni mlokole, alikuwa ni mchawi, alikuwa ni mnafiki, alikuwa ni kitu kibaya sana. Bali kwa watu walioteuliwa, waliotoka kulingana na Neno la Mungu (“Nitawatoa”), yeye alikuwa ni nabii kwao. Alikuwa ni njia ya Mungu iliyoandaliwa. Naye pia... Angalieni, walimwamini na kuepuka hukumu ya siku hiyo. Walimwamini Musa.

¹³¹ Naye alisema pia aliwajali hata akawatoa, pia Yeye akawajali safarini wakiisha kutoka. Amina. Kama vile hiyo ilivyokuwa katika maumbile ya kawaida, hii iko kwenye milki ya kiroho. Alijali! Kwa nini? Aliwapa kila kitu walichohitaji wakati wakiwa safarini. Je! aliwajali? Aliwaponya walipokuwa wagonjwa. Aliwapa uponyaji, aliwaandalia njia kwa ajili ya magonjwa yao, alimwandaa nyoka wa sha—shaba, hata wangeweza kumwangelia yule nyoka wa shaba, mfano wa dhambi, na kuponywa. Aliwalisha walipokuwa njiani, mahali hapakuwapo na chakula Yeye alishusha chakula kutoka Mbinguni. Aliwalisha. Si hivyo tu, bali aliwavisha, akionyesha Yeye huwajali wale wanaojali.

¹³² Kama wako tayari kukiri na kutubu na kuamini na kukubali, Mungu anajali! Bali huna budi kujali kwanza, huna budi kukubali yale aliyokutumia. Yeye aliwajali sana hata wangekuwa na hakika ya kwamba kusingekuwako na kosa

lolote, alimthibitisha nabii Wake kwa ishara ya Nguzo ya Moto, kuwafanya watu waone ya kwamba haikuwa tu ni mtu huyu aliyekuwa akitembea hapa, kwamba ilikuwa ni Mungu papo hapo juu yake, Yeye Ndiye aliyekuwa akiongoza njia. Mungu anawajali watu wanaojali. Mungu huwajali wale wanaomjali. Kwa hiyo alimthibitisha mtu huyu na kuthibitisha ya kwamba alikuwa ni mtumishi wa Mungu, kwa kuwatumia Nguzo ya Moto kuwaongoza kwenye nchi yenyewe. Nao walijua ya kwamba mradi tu ishara hii ya Moto huu, Nguzo ya Wingu na ya Moto ilikuwa ikiwafuata... Yeye alisema “hakuondoa Nguzo ya Moto na ya Wingu.” Yeye alikuwa pamoja nao kwa miaka na miaka nyikani, miaka arobaini. Hiyo ni kweli? Ile Nguzo ya Moto iliwaongoza! Tuko kwenye mwaka wetu wa thelathini na tatu, ikisalia miaka saba zaidi ambapo ingekuwa ni mfano ule ule. Vema, Nguzo ya Moto iliwaongoza. Yeye aliwajali. Naye aliwajali sana hata aliwafanya tu wajue ya kwamba—ya kwamba haikuwa ni kitu fulani cha kisayansi, haikuwa ni kitu fulani kilichojipenyeza, bali Yeye aliuthibitisha Ujumbe, kuuhakikisha.

¹³³ Yeye alimjali sana hata mwanamke aliyekuwa ni wa nje, sio Mwisraeli. Hakuwa mfuasi wa kundi hilo, bali alikuwa ni mtu wa nje, Mpresbiteri, Mmethodisti, ama chochote kile, alikuwa upande huo mwingine. Lakini wakati aliposikia! Jina lake lilikuwa ni Rahabu, alikuwa akiishi... alikuwa ni kahaba. Bali aliposikia jinsi ambavyo Mungu alikuwa kwenye Nguzo ya Moto na alikuwa akiwaongoza, yeye alisema acha... alimlilia Mungu, naye akawarehemu wale wapelelezi waliokuwa wamekuja kupeleleza nchi hiyo. Na kwa sababu alimjali yeye pamoja na watu wake, Mungu alimjali. Zaidi sana mpaka malaya huyu ambaye angeyatoa maisha yake kwa Kristo, kwa Huduma hiyo, kwa sababu alikuwa ameiona ishara ya Mungu wa Miujiza, naye alikuwa akitumikia miungu yake moja kwa moja kwenye dhehebu lake mwenyewe. Lakini wakati alipoiona ishara hii kuu ya Mambo ya Kimbinguni, yeye alipaza sauti na kuomba rehema, na rehema juu ya familia yake, na Mungu alimjali sana hata jiji lote likaporomoka chini, moja juu ya lingine, bali hakukuwako na jiwe moja lililotikisika nyumbani mwake. Yeye hujali! Ingawa yeye ni mtu wa nje, hakuwa kwenye kundi hilo wakati huo, lakini Yeye alijali. Daima anajali.

Alimjali Eliya wakati yeye, na yeye pekee, alipomjali Mungu.

¹³⁴ Haleluya! Hapo ndipo linapofikia. “Mtwikeni yeye fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujishughulisha sana na mambo yenu.” Petro, akizungumza na wazee wateule, wazee na hao wengine kanisani, alisema, “Mtwikeni yeye fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujishughulisha sana na mambo yenu. Wekeni kila kitu pale, kwa maana ninyi ni safi mbele za Mungu. Mna—mnatembea kama watumishi wa Mungu.”

¹³⁵ Mungu alimjali Eliya kwa sababu Eliya alimjali Mungu. Wahubiri wengine wote walikuwa wamepoteza ono la siku hiyo, walikuwa wamepoteza mapenzi ya Mungu na upendo wa Neno Lake, na wote wakawa wa kisasa. Lakini haidhuru Yezebeli aliwafanya wa kisasa jinsi gani, yule mama taifa wa nchi hiyo, haidhuru hao wahubiri wengine waliwaachilia wanawake watende na kufanya jinsi gani. Eliya alikemea hilo, katika Jina la Bwana. Yeye alijali yale Mungu aliyosema, na Mungu akajali yale Eliya aliyosema basi, maana alisema Neno la Bwana. Mungu hujali wakati unapojali, bali huna budi kujali kwanza. Naam.

¹³⁶ Angalia, Yeye alijali wakati aipomwita Eliya, kwa Neno Lake, kutoka kwenye madhehebu. Ilionekana kana kwamba ingembidi kufa kwa njaa, maana kusingekuwako na fungu la kumi na matoleo yakimjia. Lakini Yeye alimjali sana Eliya, Yeye hakumwacha afe kwa njaa wakati alipokuwa akilitii Neno la Mungu. Aliwaagiza kunguru wamlishe. Yeye alimjali Eliya kwa sababu Eliya alimjali, na Yeye ni Neno.

¹³⁷ Alimjali Danieli wakati Danieli alipolijali Neno la Mungu vya kutosha kuomba kwa uaminifu. Haidhuru mfalme alisema nini, "Sitaki hayo yafanywe tena," Eliya alivifungua tu vilango na kuangalia kukabili Yerusalemu na kuomba. Eliya alimjali Mungu, na—na Mungu akamjali Eliya. Danieli alilijali Neno la Mungu, Naye Mungu akamjali Eliya. Aliituma Nguzo ya Moto ambayo ilimshtua yule simba asimkaribie na akakesha kule chini usiku kucha. Mungu alijali kwa sababu Danieli alijali. Naam, bwana. Aliomba kwa uaminifu, akijua ya kwamba itamaanisha kutupwa katika tundu la simba kama asipotii yale maagizo ya kimadhehebu. Bali alipiga magoti karibu na dirisha, bila kuogopa yale mwanadamu alisema. Alifungua madirisha wazi kwa maana ilikuwa ni amri ya Mungu, naye akaomba kwa uaminifu na kwa moyo safi kwa Mungu wake kila siku. Alimjali Mungu na amri Yake, ndipo Mungu akageuka na kumjali Danieli na amri yake, msimamo wake. Danieli alimjali Mungu na Neno Lake, Naye Mungu akamjali Danieli na msimamo wake kwa Neno. Atafanya hivyo kila wakati. Amina.

¹³⁸ Aliwajali wana wa Kiebrania wakati walipoheshimu kwa uaminifu na kuijali imani waliyokabidhiwa mara moja, Neno la Mungu. Yeye aliwajali sana mpaka walipoipiga baragumu. . . Walikuwa na amri kutoka kwa Mungu, "Msisujudu mbele ya mungu yeyote wa kikafiri, sanamu yoyote. Msisisujudu wala kuziabudu." Hiyo ilikuwa ndiyo amri. Ndipo walipopiga baragumu na kusema "tutawatupa katika tanuru wale wasiosujudu," walijali sana hata wakaipa ile sanamu kisogo. Hiyo ni kweli. Mungu aliwashughulikia sana, hata wakati joto lilipokuja, Yeye alimtuma Mtu wa nne kule chini katika ile tanuru iliyowaka moto na kuwapoza. Yeye alijali kwa kuwa wao walijali.

¹³⁹ Kama ukitaka kushikilia kanuni fulani ya imani, Mungu hajali unalofanya. Ukitaka kufanya hivyo, Yeye kamwe hatakujali, maana unafanya yale mwanadamu aliyosema. Ila kama utalishikilia Neno la Mungu, maungamo yako ya kweli na maaminifu na kuamini Mungu ni Mponyaji, yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye atakujali.

¹⁴⁰ Yeye alijali wakati huo, aliwajali wana wa Kiebrania, Naye akawatumia Mtu wa nne kuwakomboa, ambaye alikuwa ni Kristo. Tunajua jambo hilo.

¹⁴¹ Wakati yule mtu mwenye ukoma alipopaza sauti, “Bwana!” Watu kumi wenye ukoma walitokea na kupaza sauti kwa uaminifu, “Bwana, uturehemu.” Walikuwa na ya kutosha kushughulikia haja zao, Yeye alikuwa na nguvu za kuwashughulikia. Alimjali huyo mwenye ukoma kwa kuwa mwenye ukoma alijali kufanya maungamo yao, kumwita “Bwana!”

¹⁴² Alijali, wakati yule akida alipojali nafsi yake vya kutosha kuomba apate usaidizi kutoka kwa Yesu. Wakati huyo akida alipo... alipoonyesha kwa imani yake, akazikana sanamu zake za Rumi, na akajali vya kutosha (kwa ushuhuda wa hadharani) kumwagizia aitwe aje akamponye mwanawe, Yesu alijali vya kutosha kwenda na kumponya. Yeye hujali wakati unapojali. Huna budi kujali kwanza, hata hivyo. Yeye alijali.

¹⁴³ Yeye alijali wakati Yairo alipojali vya kutosha kuhusu Yesu. Alikuwa ni mwaminio wa siri. Aliamini Yeye alikuwa mkweli, lakini kwa sababu ya msimamo wa madhehebu yake asingeweza kuja hadharani na kukiri jambo hilo, bali wakati maskini binti yake aliposhikwa na ugonjwa akafa, Yairo alijua, akiangalia kifo cha binti yake, ama kuonyesha upendo wake, alijali vya kutosha kuwakana hadharani wasioamini waliomzunguka, na kuvaa maskini kofia yake ya huduma, akaenda na akampata Yesu. Wakati Yairo alipoonyesha kwamba alijali, Yesu alionyesha alijali vya kutosha kuja na kumfufua katika wafu. Mtwikeni Yeye fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujali! Haidhuru ni kitu gani, Yeye anajali!

¹⁴⁴ Yeye alijali vya kutosha wakati hapakuwapo hata na amri ya kusema hivyo, hakuna kitu kilichosema hivyo, kamwe Yeye hakuwa ametaja jambo hilo, bali Yeye alijali kwa sababu maskini yule mwanamke asingeweza kuingia kwenye mstari wa maombi, naye alisema, “Kama ningeweza kuugusa upindo wa vazi Lake, ninamwamini.” Yeye alijali sana imani yake katika jambo hilo, hata akageuka na kumwita kutoka kwenye hilo kusanyiko, na kumwambia imani yake ilikuwa imemponya. Alijali kwa kuwa mwanamke huyo alijali.

¹⁴⁵ Yeye alijali wakati yule mwendawazimu aliyeitwa Jeshi alipojali vya kutosha, chini ya pingamizi, kujifurukuta kutoka kwenye hayo mawe ya makaburi ya pepo na akatoka kwenda

kukutana na Yesu, na kumsujudia. Wakati, Jeshi! Hao pepo kamwe wasingetoka kama Jeshi asingalijitahidi kutoka mle kukutana na Yeye. Na wakati alipojali vya kutosha kufanya jitihada hiyo, msimamo huo katika imani yake, Yesu alijali vya kutosha kutoa jeshi hili la pepo kutoka kwake, na hali yake ya wendawazimu ikaisha. Yeye alijali unapojali. Naam, bwana. Yeye hujali unapojali.

¹⁴⁶ Sasa, wakati yule kipofu alipolilia kwenye lango la Yeriko, “Ee Yesu!” Akiwa Myahudi, Mwothodoksi, mwenye sifa nzuri katika sinagogi. Lakini wakati yeye aliposema, “Hizo kelele zinazopita hapa ni za nini?”

Wao walisema, “Yesu wa Nazareti anapita, Nabii.”

¹⁴⁷ Kasema, “Yesu, Ewe Mwana wa Daudi!” Loo, hilo lilikuwa ni kemeo la jinsi gani kwa mchungaji wake na makuhani waliosimama hapo karibu. Bali hakujali yale mchungaji, kuhani, wala chochote kile kiliyosema, alikuwa na shauku! Naye alijali vya kutosha kupata kuona kwake, kwa hiyo akaita kwa sauti kuu! Na wakati mtu huyo kipofu alipokuwa tayari, naye alijali vya kutosha kuita, Yesu alijali vya kutosha kumponya. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Yeye hujali unapojali, bali huna budi kujali kwanza. Unapaswa kuthibitisha ya kwamba unajali.

¹⁴⁸ Yeye alijali sana hata wakati mwanamke, aliyeishi na wanaume sita, alipoitambua na kuijua na kuifahamu ishara Yake ya Kimasihi ya utambuzi, Yeye alijali vya kutosha mpaka akasamehe kila dhambi na kumpa yeye maji ambayo hakuja pale kuchota, kwa sababu yeye alitambua. Alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii,” wakati alipomwambia alikuwa na shida gani. Nao, alikuwa akiitazamia ile siku kuja, ila alikuwa kwenye kundi la kanisa, hakuwa na nafasi ya kufanya hivyo. Bali alipomwona Mtu ambaye angeweza kumwambia kwamba alikuwa na shida gani, alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Ninajua ajapo Masihi atafanya mambo haya.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

¹⁴⁹ Hilo latosha! Yeye alijali. Akaacha mtungi wake, na huyoo akaenda zake mjini, naye akasema, “Njoni mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyoyatenda. Haimkini Huyu kuwa Ndiye Masihi?” Alikuwa kitu kama Rahabu, yeye alijali hata akalitaharukisha jiji zima. Yeye alijali kwa sababu jambo fulani lilikuwa limefanywa, Maandiko yaliyothibitishwa yalikuwa yametimizwa na kuhakikishwa kabisa, naye alijali! Hakujali yale watu hao waliyosema ama mtu mwingine aliyosema; aliliona, alikuwapo lilipotukia. Alijali. Naye aliwajali watu wake hata akamwambia kila mmoja wao, nalo likaufanya mji mzima kumwamini Yesu Kristo. Mwanamke alijali, na Yeye alijali. Hakika, Yeye alijali.

¹⁵⁰ Yesu alijali vya kutosha kwa ajili ya Ujumbe wa siku hizi kuyatimiza mambo yaya haya kama Yeye alivyosema, mpaka

akafa na kufufuka tena kuwatumia kwa Roho Mtakatifu, yule Mfariji, kuonyesha huduma Yake leo ya kwamba Yeye angali hai. Alijali vya kutosha. Hivi sisi hatutajali? Jambo ndilo hilo, je! hatutajali? Yeye aliifia huduma hii. Alikufa kusudi Roho Mtakatifu aweze kuwa hapa siku hizi kuonyesha mambo haya. Yeye alikujali. Alijali kuuleta hapa. Alijali kutoa tamshi. Alijali kwa kuwa alikupenda. Alijali vya kutosha kufanya jambo hilo, kumtuma Roho Mtakatifu kwenye hili, kuifanya huduma hii leo.

¹⁵¹ Hivyo ndivyo Yeye alivyothibitisha ya kwamba alijali katika siku ile, kwa sababu alikuja kuthibitisha yale Mungu aliyosema angekuwa. Hiyo ndiyo sababu yule mwanamke alimtambua. Alisema, “Najua ajapo Masihi, Yeye ni Nabii. Ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya.” Unaona, alijali vya kutosha kuhusu Neno la Mungu kumthibitishia Hilo. Amina.

¹⁵² Sasa Yeye alimtuma Roho Mtakatifu, kwamba katika siku hii ya fikra za kielimu, apate kuthibitisha kwa Roho Mtakatifu yeye yule kupitia kwetu ya kwamba Yeye angali ni Masihi, alithibitishwa kwa njia ile ile. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa swali ni kwamba, je! unajali? Unawazia nini juu ya jambo hilo? Lipo hapa. Limethibitishwa tena na tena. Je! unajali vya kutosha kuliadini? Je! unajali vya kutosha kuziungama dhambi zako, kwamba umekosea? Tubu kutokuadini kwako na ulikubali. Je! unajali vya kutosha kulikubali? Yeye alijali vya kutosha kufa na kufufuka tena, kulileta kwako. Je! unajali vya kutosha kulikubali. Nafikiri limethibitishwa kote kote, tangu wakati wa Nuhu, kote kote kutoka huko Mwanzo na kuendelea. Hatuna wakati wa kuyaenda yote. Bali mnaona ya kwamba Yeye hujali, Naye alikufa ili upate kujali, ili upate njia. Naye ameileta hiyo njia. Yeye alisema vile hasa njia hiyo ingefanya, ingefanya, na sasa Huyu hapa siku hizi akionyesha kwamba ni Kweli. Sasa, katika saa hii ovu tunayoishi, je! unajali vya kutosha kuhusu jambo hilo, kwa moyo wako wote, kuliadini?

¹⁵³ Kama utaingia kwenye mstari wa maombi ama chochote kile, hilo silo, je! unajali? Mtwikeni fadhaa zenu, Yeye anajishughulisha sana na mambo yenu. Iweni waaminifu kwalo. Ninyi jalini vya kutosha kuwa waaminifu, kwa kuwa Yeye amethibitisha kwa Neno Lake lililohakikishwa kwamba Yeye anajali. Aliahidi kulituma, Yeye amelituma! Aliahidi katika Neno, Hili hapa! Yeye anajali, sasa na wewe je? Ni, inakupasa kujali, tena.

¹⁵⁴ Yeye alijali vya kutosha, alijali vya kutosha kumshinda kila adui kwa ajili yako, kwamba yote yakupasayo kufanya ni kuwa mwaminifu na kuadini. Alishinda mauti. Si kazi yangu kuishinda mauti; imeshindwa tayari. Si kazi yangu kuyashinda maradhi; si kazi ya Kristo kuyashinda; tayari yameshindwa. Inanibidi tu kujali vya kutosha kuliadini. Je! unahofu yale mtu mwingine amekwambia? Unahofu ubaini wa daktari? Unahofu yale kanisa litakayokwambia? Unahofu kusimama pale ana kwa

ana kabisa, kumkabili ibilisi? Useme, “Nimezitubia dhambi zangu, nimeweka kando kila kitu. Nimeamini kila Neno. Mimi hapa, Bwana. Umba ndani yangu kujali. Mimi... Ulinijali, ninakujali Wewe.”

¹⁵⁵ Ninatafakari juu ya ule wimbo wa kale wa kuvutia sana, “Yeye anakujali. Kupitia kwenye mwangaza wa jua ama vivuli, Yeye anakujali.”

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kamwe hatuwezi kuendelea mbele zaidi.

Anakujali,
Anakujali;
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Anakujali.

Hebu na tumwimbie, huku tumeinamisha vichwa vyetu, na moyo wetu.

Anakujali...

Hebu na tuangalie yale yote Yeye amefanya.

Anakujali,
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Anakujali.

Anajali...

Sasa, kama unajali, inua mkono wako unapoimba huo.

Anakujali;
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Anakujali.

¹⁵⁶ Baba wa Mbinguni, kwenye wakati huu katika saa iliyoenda sana ya siku, tunaungama kutoka kwenye kilindi cha moyo wetu, kwamba tunajua kwa Neno sasa kwamba Wewe daima umewajali walio Wako. Lakini shida, Bwana, hivi tunajali? Je! tunataka tu kupata elimu, kusema, “Vema, nina digrii ya udaktari, ama—ama LL.D.”? Huko ni *kujua* Maagizo ya dawa, sio kuinywa.

¹⁵⁷ Mungu, ninaomba leo ya kwamba kila mmoja wetu atazichukua huzuni za Kristo ndani ya moyo wetu, tuchukue kuteswa Kwake juu yetu, kutambua ya kwamba hatuna budi kupata pia aibu ya Jina Lake, kwamba hatuna budi kuteseka. Na jalia tuwe kama mitume wa zamani, turudi, tukishangilia ya kwamba tumehesabiwa kupata majaliwa ya kuchukua aibu ya Jina Lake. Tujalie, Baba.

¹⁵⁸ Naenda kuwaombea wagonjwa, Bwana, nikiweka mikono juu yao. Wameinua mikono yao, wengi wao, na wengi wataombewa, na wameshika kadi za maombi. Na wengine wako hapa ambao hawakuja katika wakati mzuri wapate kadi za maombi, lakini wao ni—wao ni—wao wataamini, Bwana. Wangeweza kuinua mikono yao, ilivyoonekana, kwangu mimi,

kusanyiko lote. Wengi wao ni wagonjwa. Hizi hapa hizi lesi zimewekwa hapa, tukiuhisi Uwepo Wako wa Kiungu kwa Neno lililotiwa mafuta, waponye, Bwana. Jalia kwamba ombi lao litajibiwa.

¹⁵⁹ Na sasa kutoka kwenye lesi, hadi kwenye wasikilizaji, hadi kwenye wanadamu wanaoketi huko nje wakiugua. Loo, Uwepo wa Bwana, jalia uje, Baba, na kuwaponya wote. Sivyo, asubuhi ya leo katika neema ya Kiungu, tunapokiri, Bwana...? Mimi, mtumishi Wako, ninatubu kutokuweza. Sina hata jambo moja, Bwana, ninaloweza kukupa kama matendo mema. Hatustahili. Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kufanya jambo hilo, Bwana. Hatustahili kwa mambo tutakayomba. Lakini, Bwana, tunajua ya kwamba Yesu aliondoka, akaingia juu Utukufuni, na huko anatuandalia mahali apate kuja na kutupokea Kwake Mwenyewe. Naye alitwambia ya kwamba angetutumia Mfariji, ambaye angekuwa ni Roho Mtakatifu, Naye angetenda kazi Yake na angekaa pamoja nasi milele.

¹⁶⁰ Ee Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, njoo upya asubuhi hii juu yetu, na uthibitishe Uwepo Wako, Bwana, kwa njia ile ile uliyofanya ulipotembea kwa miguu hapa duniani, kusudi kusanyiko hili lijue ya kwamba Wewe uko hapa katika siku hizi za mwisho kulithibitisha Neno Lako, na kuthibitisha ya kwamba “kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Bwana, ni kwa heshima Yako na utukufu tunaomba hili, tunapojisalimisha Kwako pamoja na maungamo yetu. Tusafishe kwa Damu Yako, Bwana. Tushe kwa maji ya Neno, na utusafishe katika Damu. Na utuweke, Bwana, kama “mifano,” kama Petro alivyosema katika fungu tulilosoma asubuhi ya leo, kwa ulimwengu usioamini. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake Yesu Kristo. Amina.

¹⁶¹ Nitamwomba dada sasa aliye na...na piano, kidogo tu. Huenda tumechelewa kidogo leo, lakini, loo, sipati nafasi ya kuja mara nyingi sana. Iweni tu na subira kwetu, kidogo, kila mtu na aketi kwa dakika chache sasa, tutamwomba kila mtu. Billy, Billy Paul, yuko wapi—yuko hapa? Uliwapa wapi, je! ulisambaza kadi za maombi? Zilikuwa zipi? B, moja mpaka mia moja. Hebu tuchukue tu chache za B tuone kama atatupa utambuzi. Vipi kuhusu hilo? Tuone kama Yeye yuko hapa pamoja nasi. Mwombeni tu, je! mnaamini Yeye atafanya hivyo? Nimehubiri na ni—nilikuwa nimetiwa upako, lakini sasa nimehubiri nje ya huo, mnaona.

¹⁶² Na hebu tuwaombe watu wasimame. Vema, tutawaombea wote, hata hivyo, hebu tuanze tu kutoka kwenye namba moja. Ni nani aliye na B, namba moja? Simama, yule aliye na kadi ya maombi. La, nitawaleta tu papa hapa karibu, waje kutoka kwenye marefu haya na washuke waje. Hebu B, namba moja, ni nani aliye nayo, kadi ya maombi namba moja? Mnataka kusema haiko humu jengoni? Vema, tutaanza... Loo, samahani,

mama. Sawa, vema. B, namba mbili, basi kama tayari tumeanza kutoka namba moja. Hebu B, namba mbili. Ni nani aliye nayo, je! waweza kuuinua mkono wako namna hiyo tupate kuuona? Njoo hapa, mama, papa hapa. Tatu, ni nani aliye na tatu? Sasa hebu tupange mstari wetu kote kote kuufuatilia ukuta huu, tusogee, ama nyuma hivyo mahali fulani. Kwa hiyo, vema, kadi ya maombi namba tatu, ni nani atakayekuja? Ni huyo mama anayekuja hapa? Sikuona mkono wako, samahani, dada. Namba nne, ni nani aliye na kadi ya maombi namba nne? Waweza kuinua mkono wako ili nione kwamba wewe ni nani? Yule mwanamume huko nyuma, yule ndugu mweusi, waweza kuja papa hapa, bwana, namba nne. Namba tano, ni nani aliye na namba tano? Wale waungwana kule nyuma, waweza kuja hapa kama u—ukiweza? Namba sita, ni nani aliye na kadi ya maombi namba sita, waweza kuinua mkono wako? Upande huu, vema, sita, bwana. Saba. Sasa, hii itawafanya kuepukana na kusongamana humu. Saba, vema, njoo moja kwa moja hapa chini, saba. Sasa namba nane, wakati tu mkininii. . . Waweza kuja, bwana? Namba tisa. Vema, bwana. Namba kumi. Vema, mvulana mdogo.

¹⁶³ Tunapowazia juu ya jambo hilo, jambo la kupendeza sana; nilipoingia, wavulana wadogo, karibu iniue nikiwazia juu ya hilo. Mvulana mdogo alisimama pale muda mfupi uliopita, akasema, “Ndugu Branham, utanifanyia jambo fulani?” Yapata tu ukubwa wa mvulana huyu mdogo.

Nikasema, “Ni kitu gani, mwanangu?”

¹⁶⁴ Akasema, “Mwombee mama yangu.” Kasema, “Yeye hulitaja tu Jina la Mungu bure, naye ana maisha mabaya sana.”

Nikasema, “Unaishi wapi? Hapa mjini?”

Akasema, “Naam, bwana.”

¹⁶⁵ Alitaka mama yake awe mwanamke mzuri. Na, si ajabu, Isaya alisema “mtoto atawaongoza.”

¹⁶⁶ Namba kumi namba, ati si namba kumi? Vema, namba kumi na moja. Vema, namba kumi na mbili, namba kumi na mbili. Vema, namba kumi na tatu, kumi na nne. Vema, kumi na tano. Kumi na tano, sikuiona, namba kumi na tano. Kumi na sita. Vema, zunguka hivyo uje, bwana, tafadhali, kumi na sita. Kumi na saba, kumi na nane. Kumi na nane, sikuiona. Vema, mama, ama dada, kumi na nane. Vema, sasa nenda huko, mama, tafadhali, tokea huko. Sasa angalieni, kama mstari wa maombi, hao wametosha kusimama kwenye wakati mmoja.

¹⁶⁷ Wakati mstari wa maombi unapoanza kupungua sana, mnaona, hebu Billy Paul ama baadhi yao hapa kutoka jukwaani. . . Ndugu Neville, Ndugu Neville, hebu Ndugu Neville baada ya kitambo kidogo, mtakapowaona. . . Sasa, mtakapoona Ndugu Neville akiona mstari wa maombi ukininii. . . ataashiria hivyo, maana nitaomba Roho Mtakatifu. . .

168 Sasa, mtu huyu, je! una kadi ya maombi, uliye kwenye kiti cha magurudumu, bwana? A—a—alikuwa na kadi yake ya maombi. Vema, sasa mnaweza kumpeleka moja kwa moja kwenye mstari wa maombi. Sasa, yupo mtu mwingine yeyote a—a—aliye hapa, ambaye huwezi kusimama? Mtu fulani na awasaidie kama wao...wakati ninii wao—wakati wao utakapofika, mnaona. Sasa, ninyi wazieni tu, anzieni mahali nilipoachia yapata kumi na nane ama ishirini, mahali fulani hapo, basi muanzie kwenye ishirini na moja, ishirini na mbili, utajua mahali pako utakapoingia.

169 Sasa je! mnajali? Je! mnaamini Yeye daima amejali? Mnaamini ya kwamba Yeye anajali sasa? Kama—kama Yeye—kama Yeye alijali wakati mmoja, Yeye daima atajali. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Naam!”—Mh.] Sasa namtaka kila mtu awe na kicho kweli, ukae mahali pako na uombe. Sasa, ninyi mlio kwenye wasikilizaji, ombeni pia. Sasa, Yeye alijali jinsi gani? Kwa sababu asingeweza kujali tena, wala hakuna mtu wala nabii, hakuna mtu mwingine anayeweza kuvuka mipaka ya kazi ya Mungu iliyoahidiwa. Hiyo ni kweli? Sasa, sijali sasa, huenda umepitia kwenye mistari ya maombi mara mia moja, lakini ninyi mnaosimama sasa na ninyi mnaoketi, ikiwa kuna dhambi maishani mwenu, kutokuamini, itubuni sasa hivi. Usithubutu kuja hapa bila hilo. Kama u—ungeweza kupitia hapa na haidhuru mtu alikuwa ametiwa mafuta jinsi gani, naye angesimama na kukuwekea mikono, hakika utaukosa ma—maili mia moja isipokuwa uamini hilo. Huna budi kuiamini. Huna budi kulikiri. Huna budi kufanya hivyo. Unaona, ndipo kama ukiangalia hapa, jinsi ambavyo kuna ninii. . . Ninatumaini mmeiona picha hiyo. Unaona? Haiwezekani kabisa kwa Mungu kutolitimiza Neno Lake kwako, kama umetimiza neno lako kwa Mungu. Unaona? Kama kweli mnaamini jambo hilo, hakuna kitu kinachoweza kuwafanya mlishuku. Wakati, anga, hakuna kitu kingine kinachoweza kuwafanya mlishuku. Mnaliamini. Je! mnaliamini? [Kusanyiko linasema, “Naam! Amina!”—Mh.]

170 Sasa, sasa nitaangalia kwenye mstari huu wote wa maombi. Nijuavyo mimi, isipokuwa iwe ni mtu huyu papa hapa, ninamjua; na ninamjua yule, ninamjua Gene Slaughter hapa chini, ninamjua; nje ya hao... nami sijui wamesimama pale kwa—kwa sababu gani. Sina fununu wako hapa kwa sababu gani. Mungu anajua. Na sasa kama ninyi nyote mnajua sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu, ninyi mnaosimama hapo. Sasa, ni wangapi katika kusanyiko hili wanajua ya kwamba sijui jambo lolote kuwahusu, inueni mikono yenu. Sasa ni wangapi wanajua kwamba Yesu Kristo anajua yote kuwahusu?

171 Na ni wangapi watakuwa radhi kusema jambo hili? Ninaamini [Kusanyiko linasema, “Ninaamini”—Mh.] kwa moyo wangu wote [“kwa moyo wangu wote”] ya kwamba Yesu [“ya kwamba Yesu”] aliniponya [“aliniponya”] wakati

aliposulibishwa [“wakati aliposulibishwa”] pale Kalvari [“pale Kalvari.”]. Hiyo ni kweli. Unaona? Sasa, kama amefanya hivyo tayari, basi ni imani yako kuukubali. Sasa, Yeye alijali vya kutosha kufanya hivyo, je! wewe unajali vya kutosha kuweka kando kila tashwishi, na kuliadini? Mtwikenii yeye fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujishughulisha sana na mambo yenu.

¹⁷² Sasa, iwapo wewe ni mgonjwa, kama unateseka, nimeona, vema, mwajua, makumi elfu mara maelfu ya mambo ambayo Roho Mtakatifu amefanya. Nanyi mnajua jambo hilo; wenye kifafa, hata kufikia kufa.

¹⁷³ Mtu mmoja alianguka akafa papa hapa jukwaani, papa hapa mbele zetu, karibu majuma matatu yaliyopita. Mkewe ni nesi aliyesajiliwa anayeketi hapa. Na mtu huyo akaanguka moja kwa moja. Yeye ameketi hapa mahali fulani. Huyu hapa mke wake ameketi hapa sasa, na—naye huyu papa hapa juu mahali fulani sasa. Naam, huyu hapa amesimama papa hapa. Macho yake yalirudi nyuma, akawa mweusi namna hiyo, ninii . . . akaanguka, nami nikashuka nikaenda pale. Alimchunguza, hamna moyo, hamna pigo. Nikaweka mikono yangu juu yake (alikuwa ameaga) nami nikaiita tu roho yake, katika Jina la Yesu Kristo, naye akafufuka. Unaona? Unaona?

¹⁷⁴ Ni kitu gani? Yeye Ndiye ufufuo na Uzima. Haikuwa ni mimi. Huyu aliyetenda kazi ni Mfariji, Roho Mtakatifu akituomba. Mnaona? Tumemkubali, sasa ni juu Yake kutuomba. Basi ningeweza vipi. . . Je! Mungu angeweza kukuokoa kinyume cha mapenzi yako? La hasha. Hawezi kukuokoa kinyume cha mapenzi yako. Huna budi kuamini.

¹⁷⁵ Sasa, hili lingekuwa ni kitu gani, kama—kama anaweza kuthibitisha, kama Mungu ataniruhusu kwa karama ya Kiungu kuwaonyesha ya kwamba Yesu Kristo yupo hapa pamoja na sisi, ya kwamba Mfariji huyu ni Yesu Kristo, Yeye ni Neno. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno.” Hiyo ni kweli? “Huyo Neno alikuwa ni Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Nayo Biblia ilisema, katika Waebrania 4, ya kwamba “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Huyatambua mawazo ya moyo.” Hiyo ni kweli? Na hivyo ndivyo Yesu alivyofanya kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno lililotiwa mafuta, Masihi. Loo, jamani! Hivi hamlioni hilo? Masihi ni nini? Aliyetiwa mafuta. Kitu gani kilichotiwa mafuta? Neno lililotiwa mafuta! “Nalo Neno lilifanyika mwili.” Yeye alikuwa Ndiye hilo Neno lililotiwa mafuta! Unaona jambo hilo, Ndugu Vayle? Unaona, Yeye Ndiye Neno lililotiwa mafuta!

¹⁷⁶ Na sasa wakati unapojikabidhi mwenyewe Kwake, basi Yeye anakutumia zaidi ya vile unavyojua, akithibitisha ya kwamba Yeye angali ni Neno lililotiwa mafuta, Mtambuzi wa mawazo ya moyo. Loo, mtu, mtu yeyote anawezaje kulitilia shaka? Aminini tu. Msitie shaka. Na sasa ninyi mnaoketi huko nje, ni—nililigusia somo hilo asubuhi ya leo. Wakati maskini mwanamke mmoja

alipohofu ya kwamba hangeingia kwenye mstari wa maombi, labda, bali akagusa upindo wa vazi Lake Naye akageuka. Mnaamini hilo? Mnaamini linaweza kufanywa tena leo? Naam. Sasa, ungeigusaje?

¹⁷⁷ Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi Kuhani Mkuu, ameketi mkono wa kulia wa Ukuu wa Mungu, kutuombea tunapokiri. Tunaungama tunamwamini, nasi tunataka kumgusa Kuhani mkuu. Nasi tukingusa, Yeye angefanya nini? Yeye yupo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu. Ndipo angeweza kujibu moja kwa moja na kukwambia vile vile hasa. Hiyo ni kweli? Sasa ninyi aminini hilo na mwendelee tu kuketi, mnyamaze, iweni na kicho na mwangalie. Sasa, kama Yeye atafanya jambo hilo angalau mara tatu, hiyo itatosha, siyoy? Mara tatu, kama atalifanya. Moja, mbili, tatu, kama atafanya hivyo.

U hali gani?

¹⁷⁸ Sasa, hebu kidogo wakati tunapoomba tu. Unaona, hii ni, sininii... Hili ni jambo ambalo kidogo ni tofauti sasa hivi; nimekuwa nikihubiri, kisha nikageukia jambo hili. Sasa, sijamwita Bwana kwa ajili ya jambo hili kwa muda mrefu, bali Bwana Mungu anaujua moyo wangu, na ayajibu maombi yenu. Nami ninaamini jambo hilo, ya kwamba Yeye atalifanya.

¹⁷⁹ Sasa, huyu hapa mwanamke amesimama, hatufahamiani. Nijuavyo mimi, sijapata kumwona maishani mwangu. Huenda ameketi kwenye wasikilizaji mahali fulani ama alinijua kwa vitabu, bali Baba wa Mbinguni anajua, nijuavyo mimi, kamwe sijapata kumwona kwa macho maishani mwangu. Hatufahamiani.

¹⁸⁰ Sasa, kama Yeye ni yeye yule, huyu hapa mwanamume na mwanamke wakikutana hapa kama vile Yesu alivyokutana na yule mwanamke kisimani, ambaye nilinena habari zake muda mfupi uliopita. Yeye alimjali. Sasa, mwanamke huyu labda hawana hatia ya kitu kile kile alichokuwa nacho mwanamke huyo, bali kuna kasoro. Lakini yeye anamjali kadiri anavyomjali mwanamke huyo. Unaona, Yeye anajali. Sasa, na wakati alipoliona, yeye alilitambua. Sasa sisi hapa wawili tumesimama namna hii. Sasa, sijapata kumwona.

¹⁸¹ Sasa, kama Roho Mtakatifu aliye mkuu, asiyeonekana, sasa kama hisi za imani zitamtangaza kwangu. Yeye ameleta hisi za imani, na Neno Lake limezileta karibu sana katika siku hizi za mwisho mpaka Yeye ana picha Yake pale. Yeye ameileta karibu sana na hisi zetu, akazitia mafuta, ameondoka na kumwona akija hapa ndani na kuzunguka kote kote katika mfano wa Nguzo ya Moto. Siyoy? Sasa Yeye yupo hapa, ninajua Yeye yupo hapa. Imani yangu inasema Yeye yupo hapa. Sasa kama anaweza tu kujifanya mwili vya kutosha hapa ndani kuyashika maisha ya

mwanamke huyu, mnaona, kama alivyoahidi angefanya. Roho Mtakatifu angefanya kazi zile zile alizofanya.

¹⁸² Sasa mimi, kwa kuwa nimekuwa nikihubiri, ninataka tu kuzungumza nawe kwa dakika moja kusudi nione tu.

¹⁸³ Kama alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, Yeye alisema, “Nipe maji ninywe.” Mnajua, Yeye alikuwa tu... Labda alikuwa ameketi pale akiwazia juu ya kuondoka kwenda kutafuta chakula, halafu i—ilimbidi kuzungumza naye kwa dakika moja, mwajua. Baba alikuwa amempeleka huko juu. Ilimbidi kwenda. Alikuwa akienda Yeriko; naye akapanda kwenda Samaria, hiyo ni huko juu mlimani, alikuwa na “haja ya kupitia kule.”

¹⁸⁴ Vema, kwa njia moja ama nyingine, nilikuwa na haja, Baba alinituma kutoka Arizona, hapa, nawe ukaingia. Kwa hiyo yote ni mamoja tu. Hakuna kitu kinachotukia kwa bahati, yote yanatukia kwa kusudi fulani. Neema ya Mungu, ni kweli.

¹⁸⁵ Sasa, nikiwa sikujui wewe, nawe unaonekana mwenye afya kweli, na huenda hilo silo lililokuleta hapa. Huenda ikawa ni kitu kingine. Huenda ikawa ni mpendwa wako, huenda ikawa ni mambo ya nyumbani, ya kifedha. Sina njia ya kujua, unajua hilo. Bali kama Yeye atanielezea lililokuleta hapa, utajua kama ni kweli ama si kweli. Na je! wasikilizaji wataamini kwa moyo mmoja basi? Sasa unatusikia, na unarekodiwa, nasi tunasimama tu hapa jukwaani.

¹⁸⁶ Mama huyu, ninamwona akikiinua kichwa chake juu namna hii. Yeye ana, yeye anasumbuliwa na kuumwa na kichwa, kama kipandauso. Ni kuumwa na kichwa mfululizo. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Hiyo ni kweli. Jambo lingine, yeye ana ugonjwa wa kikoromeo, ambao ameambiwa, kwa vyovyote vile, ambao—ambao unakusumbua, naye amesema kweli, ni kikoromeo. Halafu una matatizo tu, una shida nyingi tu; wasiwasi, fadhaa, unashikwa na mahangaiko, “mara nyingine sijui nimesimama wapi, na kama niko ndani ama nje.” Na hiyo ni kweli. Ni ukweli. Sasa, Yeye anakujua, usingeweza kujificha sasa hata ufanye nini. Unaona? Unaamini anaweza kuniambia kwamba wewe, wewe ni nani? Vema, Viola, wewe rudi nyumbani, Yesu Kristo anakupa afya.

Unaamini?

¹⁸⁷ Mimi sijui. Yesu Kristo anajua mambo yote. Ni mgeni mwingine kwangu. Mungu anatumia sote wawili. Je! unaamini mimi kwamba ni nabii Wake, mtumishi Wake? Unaamini kwamba mambo haya ambayo nimeyahubiri kutoka kwenye Neno hili ni Kweli? Unaamini? Kama Bwana Yesu ataniambia uko hapa kwa sababu gani, wewe niamini mimi kuwa ni mtumishi Wake. Naye anafanya jambo hili kwa sababu anakujali. Yeye, Yeye anakujali, Yeye anafanya hivyo kwa sababu anakujali. Anawajali hawa wengine ambao wamekuja

mstarini. Yeye anawajali. Umekuwa na shida, ajali, ajali ya motokaa. Umeshtushwa sana nayo. Hiyo ni kweli. Una shida ya kiungo chako. Hiyo ni kweli. Utapona, na wasiwasi utakuondokea, kwa hiyo nenda zako tu nyumbani, ukimshukuru Bwana, na kusema, “Bwana asifiwe!”

“Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Vema.

¹⁸⁸ Je! unaamini? Sikujui, hatufahamiani. Bali Mungu anakujua. Je! unaamini Yeye anaweza kuniambia sababu ya wewe kuwa hapa, ama kitu fulani kingine kukuhusu wewe? Ungeamini? [Mwanamke huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Yupo mwanamke mwingine. Haikuwa ni wewe, unaona. La, sivyo. Ni wewe, uko hapa kwa ajili ya mtu fulani. Unamwakilisha mwingine, ni mama yako. Hiyo ni kweli. Ana shida fulani kwenye kiungo chake, pia. Hiyo ni kweli. Yeye hayuko hapa. Yuko karibu na mahali panapoonekana kama, panaonekana kwangu kama ni Kiingereza, karibu, mahali fulani hapa chini. Wewe, hiyo ni kweli, unaamini? Vema, nenda zako. Ameponywa. Nenda zako tu.

¹⁸⁹ Kulikuwako na wanawake wawili. Mmoja wao alikuwa ni mzee zaidi, kwa hiyo mimi—mimi nilishangaa ilikuwa ni wapi. Niliangalia kuona mahali—mahali ilipokuwa. Bwana Mungu anajua mambo yote, sivyo? Naye anaweza kufanya mambo yote. Je! mnaamini jambo hilo? Amina. Yeye si ni wa ajabu? Ninampenda. Yeye, Yeye Ndiye Uzima wangu. Yeye Ndiye yote niliyo nayo. Yeye Ndiye yote ninayohitaji. Endelea tu, Yeye alikufanya mzima, bwana.

¹⁹⁰ Upako ulimfuata mama huyo. Kuna mama mwingine anayeketi pale anayesumbuliwa na wasiwasi, naye ana kivimbe chini ya mkono wake. Hiyo ni kweli? Alipoweka mikono yake juu yako wakati huo, ulisikia hisi ya ajabu kweli. Hiyo si ilikuwa ni kweli? Hapo ndipo Yeye alipokuponya. Utakuwa mzima. Yesu Kristo. Angalieni mahali alipo. Mwanamke aliyekuwa akiomba, ama hapa, mnaona. Je! mliona wakati alipokuwa akiomba, nilipokuwa nikimwomba, ni jambo gani lililotukia? Mnaona? Nilimwona mwanamke mwingine, nami nikaangalia kule. Kulikuwako na hisi kuu. Hapana budi wanafahamiana, kitu kama hicho, ama wanajuana, maana mwanamke huyo alikuwa akimhurumia mwanamke huyu hapa. Kisha mwanamke huyu anashuka anaenda anamgusa, na, alipofanya hivyo, niliangalia nikaona kitu fulani huko ng'ambo, naye huyo hapo amesimama pale. Kamwe sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Mungu Mbinguni anajua hivyo. Loo, jamani! Kwa nini utilie shaka?

¹⁹¹ Kama unaweza kuamini, Yeye hata angeweza kukuondolea tabia mbaya. Unaamini hilo? Unaamini atakuponya? Nenda zako, nawe utaachana nayo sasa hivi wala hutavuta sigara

nyingine. Nenda zako, na uamini kwa moyo wako wote. Mwamini Mungu. Usitilie shaka.

¹⁹² Je! mnaamini? Tumekuwa na watatu tayari? Mwaminini Mungu. Msitilie shaka. Aminini tu. Mnaamini upako upo hapa sasa? [Kusanyiko linasema, “Ndiyo. Amina.”—Mh.] Amina. Msitilie shaka. Aminini!

¹⁹³ Nitakuwekea mikono, na uamini. Utaamini pamoja na mimi? [Mwanamume huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Katika Jina la Yesu Kristo, naomba ndugu huyu aponywe. Amina. Kuwa na imani sasa, usitilie shaka. Hebu kidogo.

¹⁹⁴ Kuna jambo fulani lililotukia huko kwenye wasikilizaji wala nisingeweza kuliona, liko moja kwa moja hapa nyuma. Nafikiri limefichwa kwangu sasa hivi. Hili hapa. Ninaliona katika kivuli. Ni mwanamume fulani, naye anaugua wasiwasi. Ana mvulana aliye na kifafa. Amini kwa moyo wako wote, bwana. Unaamini? Basi. Vema, weka mkono wako juu ya mvulana huyo hapo naye atakuwa mzima. Amina. Bwana asifiwe.

¹⁹⁵ Je! mnaamini? Huyo pepo alidhani angeweza kujificha kutoka kwa huo, bali alishindwa. Mnaamini? Kitu hicho kingali kinasogea mahali fulani. Loo, jamani, kwa neema na kujali! Kuna mtu mwingine mwenye kifafa mahali fulani hapa. Naam, huyu hapa papa hapa. Unaamini? Kuwa na imani. Unaamini Mungu anakuja? Unaweza kurudi Ohio, uwe mzima, Bw. Nelson T. Grant. Hilo ndilo jina lako. Kama utaamini, vitu hivyo vitakuacha wala havitakusumbua tena. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu, sijui lolote kumhusu.

Huwezi kulificha sasa, Roho Mtakatifu yupo hapa!

¹⁹⁶ Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu na tumpe Mungu sifa. Bwana Yesu, tunakushukuru. Ni wewe yule jana, leo, na hata milele. Neema yako kamwe haishindwi, Bwana, ni ile ile wakati wote. Ninaomba ya kwamba rehema Yako kuu na fadhili zitakaa juu ya watu hawa. Ulijali vya kutosha. Bwana, kuja na kujithibitisha Mwenyewe. Wewe ni Mungu. Wewe Ndiye Mtakatifu mkuu, Roho Mtakatifu mkuu. Sasa jalia watu hawa waamini, Bwana, wanapopitia hapa, na kila mmoja wao aponywe. Kwa kuwa upako Wako upo hapa, ninajilaza mwenyewe juu ya lesu hizi. Ninaomba, Bwana, ya kwamba utatujalia maombi haya, Baba. Tujalie, Bwana, kote hapa katika wasikilizaji.

¹⁹⁷ Na jalia kila mtu aliye kwenye Uwepo wa Kiungu ajali vya kutosha kuamini kwamba Wewe ulijali vya kutosha kutokea katika siku ya mwisho miongoni mwa watu Wako, na kuthibitisha! Huwezi kuwaponya, Bwana, huwezi kufanya yale ambayo umefanya tayari. Uliwaponya tayari. Na hili ndilo jambo pekee linaloweza kufanywa, kuwafanya waamini. Nawe unajali vya kutosha, ingawa kuna kutokuamini kwingi tunakoyumbayumba kwake, Wewe ungali unajali vya kutosha

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu dada yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, mponye dada yangu.

Ndugu, Yeye anajali. Nawe je? Katika Jina la Yesu, pona!

202 Kila mtu katika maombi sasa, kila mtu aombe. Hawa ni watu wenu wakipitia hapa.

203 Katika Jina la Yesu, mponye dada yangu. Katika Jina la Yesu, mponye huyu ndugu yangu. Amina. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu ndugu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu. Katika Jina la Yesu, mponye dada yangu mdogo. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu dada yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu dada yangu, Bwana. Katika Jina la Yesu, mponye huyu dada yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu dada yangu, ndugu yangu. Mponye huyu dada yangu. Mponye huyu dada yangu, Bwana. Mponye huyu dada yangu, naomba katika Jina la Yesu. Mponye dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu. Mponye dada yangu, katika Jina la Yesu.

204 Dada, Yeye anajali. Nawe je? Katika Jina la Yesu, pokea uponyaji wako. Katika Jina la Yesu, pokea uponyaji wako, dada. Katika Jina la Yesu, pokea uponyaji wako. Katika Jina la Yesu Kristo, pokea uponyaji wako. Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu dada yangu. Mponye huyu dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu. Mponye huyu ndugu yangu, katika Jina la Yesu. Mponye huyu dada, katika Jina la Yesu. Mponye dada yetu, katika Jina la Yesu. Mponye ndugu yangu, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Mponye dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu. Mponye huyu ndugu yangu, katika Jina la Yesu. Mponye dada yangu, katika Jina la Yesu. Mponye dada yangu, katika Jina la Yesu. Mponye mvulana huyu mdogo, katika Jina la Yesu. Mponye huyu mvulana mdogo, katika Jina la Yesu. Mponye Ndugu Creech, Bwana, katika Jina la Yesu. Mponye huyu dada yetu, katika Jina la Yesu. Mponye huyu ndugu yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Waponye, Baba, wote wawili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

205 Mungu akubariki, ndugu. Je! huyo ni mtoto wako? Mke wako? Vema, sikujua jambo hilo. Bwana akubariki, ndugu. Mponye huyu ndugu yangu, katika Jina la Yesu. Mponye huyu dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu. Mponye huyu dada yangu, katika Jina la Yesu. Mponye huyu ndugu yangu, katika Jina la Yesu. Mponye huyu dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Mponye huyu ndugu yangu, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Mponye huyu dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Mponye huyu dada yangu, katika Jina la Yesu. Waponye, Baba, katika Jina la Yesu.

²⁰⁶ Ninaomba ombi langu aminifu, kila mmoja. Mnajali sasa. Yesu anajali. Yesu alituma Ujumbe. Yesu alimtuma Roho Wake. Yesu alilituma Neno Lake. Yesu alimtuma mtumishi Wake. Sote tunajali. Sasa na wewe je? Kama unajali, liamini, likubali kwa uaminifu, litatimizwa.

Katika Jina la Yesu, mponye ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye huyu, dada yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye dada yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye ndugu yangu.

²⁰⁷ Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yangu. Tujalie hilo, Baba.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu.

Katika Jina la Yesu, Mponye huyu, dada yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu.

Bwana, katika Jina la Yesu, mponye huyu, ndugu yangu.

²⁰⁸ Ee Mungu wa Mbinguni, rehemu ili uponye; tujalie, Bwana. Jalia nyama na nguvu zije katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, ndugu yangu.

Mungu, dada yetu hapa kwenye kiti, naomba ya kwamba Wewe umponye na umfanye mzima, Bwana, katika Jina la Yesu.

²⁰⁹ Mungu, mponye dada yetu hapa, katika tendo lake zuri la wema, msaidie mwanamke huyu, katika Jina la Yesu.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yangu.

Mungu, mponye ndugu yangu, naomba, katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu mama mzee.

Katika Jina la Yesu Kristo mponye mwanamke huyu.

Katika Jina la Yesu mponye . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye . . . ? . . . Bwana.

Katika Jina la Yesu, mponye ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye huyu, Bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yangu, Bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye . . . ? . . .

Mponye ndugu yangu katika Jina la Yesu Krsito.

Mponye ndugu katika . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

210 Njoni kwa unyofu wote; msitilie shaka chochote; liaminini tu. Kila mtu akiomba sasa. Hawa ni watu wetu wakipitia hapa, watoto wa Mungu. Amini.

Mponye maskini dada yetu, Baba, katika Jina la Yesu.

211 Mponye rafiki yangu wa thamani, Bwana. Mungu, amengojea kwa muda mrefu sana; jalia hii iwe ndiyo saa yenyewe. Amina.

Katika Jina la Yesu, mponye huyu...?...

Katia Jina la Yesu...?...

Katika Jina la Yesu, mponye, Baba.

Katika Jina la Yesu, mponye...?...

Katika Jina la Yesu, mponye, Baba.

Katika Yesu Kristo...?...

Katika Jina la Yesu, tunaweka mikono yetu juu ya...?...

Katika Jina la Yesu, mponye...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu.

Mponye dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu.

Katika Jina la Yesu, mponye ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye huyu ndugu yangu, Bwana.

Katika Jina la Yesu, mponye dada yangu, Baba.

Kati Jina la Yesu...?...

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu.

212 Mungu, katika Jina la Yesu, ondoa kupooza kutoka kwa ndugu yangu, Bwana, mfanye mzima, Baba.

Mungu, katika Jina la Yesu, mponye huyu, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye huyu, shemeji yangu, ninaomba.

213 Katika Jina la Yesu, mponye huyu, dada yangu, Bwana; Mungu mponye, katika Jina la Yesu Kristo.

Mponye dada yetu, Baba, katika Jina la Yesu Kristo...?...

214 Ee Mungu, sasa, hapa pana baadhi ya maombi, jalia yawe hivyo, katika Jina la Yesu.

215 Sasa, hiyo ndiyo njia ya kuupokea, ndugu. Sasa, kwa kuwa Bwana ameufanya.

216 Hebu angalia ikiwa mtoto huyo si...?...Sasa, yeye huniwezesha kujua shida uliyo nayo. Mimi siitaji tu...?... katika Jina la Yesu Kristo...

217 Ee Mungu, hapa amesimama...?...anasimama hapa kwa niaba ya Edith. Tunawazia kuhusu maskini huyo, Bwana. Alikuwa hapa ili kusukumwa, hivi sasa tu. Dada yake anasimama kwa niaba yake, Bwana. Jalia, Ee Mungu, jalia maombi haya, katika Jina la Yesu, kwa ajili yake.

218 Mungu, mrehemu ndugu yetu na umponye, Baba, katika Jina la Yesu.

219 Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mguse huyu, ndugu yangu wa thamani na umpe afya, Baba.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, Bwana, mponye dada yetu.

Mponye ndugu yetu, Baba, katika Jina la Yesu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yetu.

Ee Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu . . . ? . . .

Mungu, mponye huyu mvulana mdogo, katika Jina la Yesu Kristo.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yetu, Bwana.

Katika Jina la Yesu, mponye nanii wetu . . . ? . . .

Ee Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye . . . ? . . .

Mponye dada yetu . . . ? . . . katika Jina la Yesu.

Ee Mungu, mponye huyu, dada yetu, naomba, katika Jina la Yesu.

Mungu, mponye dada yetu, kwa kuwa ninaomba katika Jina la Yesu.

Mungu, mpe afya; tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu.

220 Mungu, mguse ndugu yetu; ni Neno Lako; uliliahidi, Bwana, na sisi tunakuja tukiliamini, katika Jina la Yesu.

221 Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu, Bwana; amekuwa kwa unyofu, akiamini sasa; jalia aende na kuwa mzima.

Katika Jina la Yesu jalia aende na aponye, Bwana.

222 Mungu, iweke mikono Yako ya uponyaji juu ya . . . ? . . . jalia warudi nyumbani kwake na kile alichomba. Ee Mungu, jalia uponyaji, Bwana.

Mponye dada yetu, Baba, katika Jina la Yesu.

Mponye dada yangu, katika Jina la Yesu.

Mungu wa Mbinguni, mponye ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo.

Na dada yangu, katika Jina la Bwana Yesu.

Mponye huyu . . . ? . . . katika Jina la Yesu.

Mponye huyu dada yangu Daulton, katika Jina la Yesu.

Mponye dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu.

Mponye ndugu yangu, Bwana, katika Jina la Yesu.

223 Sasa, Yeye hujali; nawe pia, ndugu. Nenda ukampe sifa na kumshukuru, katika Jina la Yesu Kristo . . . ? . . . Jalia, Bwana,

mizigo yake imekuwa mingi; ifanye myepesi sasa, Baba, katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yetu.

224 Nakuomba utume rehema juu ya mwanamke...?...

225 Mungu, jalia uponyaji wa dada yangu, hapa. Ninamwona akisimama mlangoni, anangojea, Roho Mtakatifu amemzunguka. Mungu, jalia aende na kukuamini Wewe. Tujalie, Baba.

Katika Jina la Yesu, jalia awe huru, Baba.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo...?...

Katika Jina la Yesu, naomba ya kwamba Wewe utamponya dada yangu.

Katika Jina la Yesu, mponye huyu, dada yangu.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yangu.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo...?...

Mungu, mpe ndugu yangu afya, katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu...?...njoo karibu...?...nguvu zitamponya.

226 Ee Mungu, mponye...?...na umwonyeshe mwanamke huyu...?...mahali hapa. Lifanye likolee, Bwana, na jalia ahisi nguvu za Mungu, katika Jina la Yesu...?...

Mungu, mponye ndugu yetu, Bwana, na jalia awe mzima.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu, Mungu.

227 Mungu, mponye...?...mwanamke huyu amekuona Wewe ukifanya mengi sana. Jalia sasa wote watakuwa...?...

Ponya...?...Bwana, naombea rehema, mpenzi Bwana Yesu.

228 Mungu, mponye huyu...?...mpe afya mwanamke huyu...?...Bwana, na masikitiko yake yamekuwa ni mengi nasi twayashiriki. Sasa, jalia awe...?...

Katika Jina la Yesu, mponye huyu, dada yangu, Bwana.

Mponye ndugu yangu katika Jina...?...

Mungu, mponye huyu ndugu yangu, na umpe afya...?...

Mponye dada yetu, Bwana, katika Yesu Kristo...?...

Mponye dada yangu, katika Jina la Yesu.

Mponye ndugu yangu mdogo, katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu, mponye huyu, ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, ndugu yangu.

Mungu, mponye dada yangu. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe.

229 Mungu, mponye huyu, ndugu yangu, mjalie, katika Jina la Yesu Kristo awe...?...

Ee Mungu, mponye dada yangu katika Jina la Yesu Kristo.

²³⁰ Mponye dada yangu hapa, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aende na...?...

²³¹ Mungu, mjalie anachoomba, katika Jina la Yesu Kristo, naomba ya kwamba umjalie hicho anachoomba.

²³² Mungu, Dada Simmon, jalia neema na rehema ya Mungu, hebu jinsi alivyoingojea saa hii, wakati ambapo anaweza kuuweka chini...?... Na jalia aponywe...?...

²³³ Mungu, Ndugu Ungren...?... Mungu, ana sauti nzuri sana, akitangaza Injili. Mdumishe na afya njema, Mungu; jalia hilo, katika Jina Yesu.

²³⁴ Mungu, Dada yetu Kidd analiitia hilo Jina la...?... Ninaomba ya kwamba nguvu Zako zitamweka huru sasa...?... kwa unyofu maskini mama huyu...?... katika siku saba anapaswa kuwa pamoja na mama yake. Jalia hilo, Baba, katika Jina la Yesu Kristo.

²³⁵ Mungu, kwa ajili ya watoto wake, Ee Mungu, wanazurura, na wengi wao ni wagonjwa, na huyo msichana ni mgonjwa, na...?... Ee Mungu, ninaomba ya kwamba utatujalia hayo, kupitia Jina la Yesu Kristo.

²³⁶ Ninashukuru sana kwa ajili ya Ndugu Tom, Bwana, naomba ya kwamba utamponya na kumsaidia. Libarikiwe Jina...?...

²³⁷ Yupo mtu hapa chini...?... Je! ungependa kuombewa pia, ndugu? Bwana Yesu...

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Anakujali,

Anakujali;

Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,

Anakujali.

Anakujali,

Mtwikeni tu fadhaa zenu, basi.

Anakujali;

Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,

Anakujali.

²³⁸ Je! mnamjali? Mnalijali Neno Lake? Amina. Bwana awabariki. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi. Ninaamini nilijibu haja hizi. Nilizijibu haja, sivyo, kila mmoja wenu.

²³⁹ Muda mfupi uliopita nilifanya kosa dogo mkutanoni, nina hakika mtu fulani aliliona. Naye Bwana amenionyesha hilo sasa hivi mahali fulani. Nilimwambia mtu mmoja jambo fulani huku nikilikusudia mtu mwingine. Si—siwezi kumwona mtu huyo mahali alipokuwa, bali ilikuwa ni mtu fulani ambaye niliawekea baraka juu yao kwa ajili ya mtu mwingine. Nami... Walikuwa wakipita upesi sana, nami sikuwa nikiona.

Wala sikuninii... Naam, ndivyo ilivyokuwa, naliona sasa. Ni mwanamume huyu na mwanamke huyu wanaoketi papa hapa. Kama sikosei, niliwapa mkono jana usiku kwenye—kwenye—kwenye chumba cha moteli, ama kitu kama hicho, kwenye uwanja wa moteli, hapa juu kwenye Jefferson Villa. Nilimwambia mwanamume huyu jambo fulani, nikasema “dada” badala ya “ndugu,” mlipopitia hapa. Mliona jambo hilo? Nililikusudia kwa mke wako. Sasa, amekuwa na shida kwa kipindi fulani, shida ya utumbo kwa muda mrefu. Mmetoka Illinois. Bibi Mongaland, hiyo ni kweli, hilo ndilo jina lako. Sasa, unajua mimi sikukujua, bali uko moja kwa moja kwenye mawasiliano sasa. Wewe amini kwa moyo wako wote, na utajisaidia vizuri kabisa kama kawaida yake, kama utaamini. Upate kuona ya kwamba wakati wote, sasa mimi. . .

²⁴⁰ Jambo pekee nijualo, jana usiku ninakumbuka nikifikiri mtu huyo, nilifikiri alikuwa na nywele nzuri sana, akiipiga nywele yake wei katikati, mtu huyu mwenye mvi anayeketi hapa. Ilitokea tu niliangalia, na kulikuwako na ile Nuru ikiangaza juu yao namna hiyo. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Ndipo nikalionga hilo ono likitokea. Sijui walikuwa ni nani ama chochote kile juu yake. Bibi huyo alikuwa huko nje jana usiku, nikasema, “Je! unakuja mkutanoni?” Akasema, “Ndiyo.” Lakini neema ya Mungu ikalivuta moja kwa moja tena, naye alikuwa ndiye. Je! uliliona hilo kwenye mstari wa maombi, ndugu, ya kwamba jambo fulani lilisemwa ambalo lilienda kwingine? Lilikuwa linasemwa kwa dada wala si kwako. Hilo, hilo lilikuwa ni sawa, lilimwendea da—dada pale.

²⁴¹ Sasa ili kwamba mjue hilo, kupitia kwa mstari huo wa maombi, yule Malaika wa Bwana alikuwa pale. Angeweza kuita. Lakini mnapoita, inadhoofisha, inadhoofisha, inadhoofisha. Mnaona? Kwa hiyo Yeye anawajali, na mimi—mimi ninawajali. Ningaliendelea tu na wanne ama watano zaidi, na halafu, muda si muda mwajua, Billy amekuwa hapa akiniondoa mimbarani. Lakini nilifikiri kama, hakika, ni—nimeishi hapa pamoja nanyi nyote miaka hii yote, na huku na huku kote nchini, ninyi—ninyi mnajua ninawapenda. Loo, ninawapenda kana kwamba mlikuwa ni watoto wangu binafsi, nanyi ni watoto wangu katika Injili. Nimewazaa kwa Kristo, kwa njia ya Injili. Na sasa ninafikiri hizi, haja hii na kadhalika hapa, nimejibu.

²⁴² Sasa, ninawapenda. Nami nilifikiri, kama nilienda na kuwawekea mikono, nanyi mkaona ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa akifanya jambo hilo, halafu vurugu kidogo ikaanza mkutanoni kwenye mstari namna hiyo. Nililikosa, wakipita upesi sana, ndipo nikaitamka baraka moja kwa mwingine, ndipo Roho Mtakatifu akageuka moja kwa moja baada ya mkutano kwisha na kulionyesha moja kwa moja tena. Mnaona? Hivi hamwoni, Yeye hujali! Sasa nanyi je! mnajali? Mnajali vya kutosha kusema, “Tangu sasa na kuendelea, kuna kitu moyoni

mwangu kinachoniambia ya kwamba shida zangu zimekwisha. Mimi ni—mimi ni mzima, nitapona”? Mnaamini hilo? Inueni mikono yenu, “Ninaamini Hilo!” Mungu awabariki.

Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Yeye anakujali.

²⁴³ Hii ni karamu kubwa mno tu ya upendo. Hebu tuuimbe na kupeana mikono mmoja kwa mwingine.

Yeye anakujali,
Yeye anakujali;
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Yeye anakujali.

²⁴⁴ Nimewaweka kwa muda mrefu sana asubuhi ya leo mpaka mimi—mimi... Mchungaji wangu hahubiri kwa muda mrefu kama ninavyohubiri. Atajaribu kuwaletea ujumbe usiku wa leo, nasi tutawajulisha kama kutakuwako na ibada ya Jumapili ijayo chini ya ninii... jina hilo. Kama nisipoweza, kutakuwako na ibada haidhuru. Kwa hiyo ninyi nyote, Bwana awabariki, kila mmoja. Nafikiri kuna ibada ya ubatizo inayokuja sasa hivi.

²⁴⁵ Kwa hiyo kama mtasimama tu kwa muda kidogo, kwa ajili ya kuwaruhusu mwondoke. Hebu na tuuimbe huo tena. “Mtwikenii yeye fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujishughulisha sana na mambo yenu.” Na sasa kama mnamjali, hebu na tuseme, “Bwana, mimi...” Mnapofanya jambo hili, mna—mnatoa tamshi hili, “Bwana, ninajua unanijali. Nami ninaiinua mikono yangu, ninakujali Wewe.” Na hebu tuinue mikono yetu kwenye karamu hii ya upendo wa fadhila, tunapoimba.

Anakujali,
Anakujali;
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Anakujali.

²⁴⁶ Sasa tunapoviinamisha vichwa vyetu, semeni... [Ndugu Branham anauvumisha *Anakujali*—Mh.] Loo, utamu wa Bwana wangu! Hivi huusikii upendo Wake ukikuvuta moja kwa moja karibu na Yeye? Sema, “Pia, Bwana, ninakupenda. Ninakupenda. Unanijali mimi, Bwana. Ulijali sana mpaka wakati nilipokuwa mwenye dhambi Wewe ulinifia. Ulijeruhiwa kwa makosa yangu, kwa kupigwa Kwako niliponywa.”

Anakujali,
Anakujali;
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Angali anakujali.

²⁴⁷ Kumbukeni tu hilo sasa mnapoviinamisha vichwa vyenu. Nitamwomba Ndugu Edwards hapa kama ataturuhusu tuondoke kwa maombi. Lakini, kwanza, hebu na tuuvumishe huo tena. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Anakujali*—Mh.] Kumbukeni, mwangaza wa jua ama kivuli, Yeye angali

anajali. Alijali. Je! wewe unajali? Sema, “Naam, Bwana, ninaahidi ninajali. Ninaendelea moja kwa moja sasa. Tangu sasa na kuendelea, ninajali. Ninaujali ushuhuda wangu.” [Ndugu Branham anaendelea kuvumisha *Anakujali*.] “Anakujali.” Ndugu Edwards.



YEYE HUJALI. JE! WEWE UNAJALI? SWA63-0721

(He Cares. Do You Care?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 21 Julai, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org